# Nipashe

Ijumaa Februari 17, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581224

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Aangua** kilio baada ya kusomewa mashtaka

UKURASA 3





UKURASA 11

# Kauli ya Muliro yaibua mjadala



• **Ni** kuhusu raia kuomba lifti kwenye 'difenda'...*Endelea ukurasa 2*




## Prof. Lipumba anusurika kifo njiani kwenda mkutanoni

UKURASA 3


REACH A WIDER AUDIENCE THIS Valentine SEASON

AT AN AMAZING OFFER UP TO 25% Off

On valentine season advertisements*

FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023

The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY

Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com

*Terms and conditions apply.

Followus: @Theguardiantz


# Wadau wapongeza mikopo wanafunzi elimu ya ufundi

UKURASA. 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA WABANANA BETIKA MTOKO UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mufti wa Tanzania, Shehe Abubakari bin Zuberi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuzindua tume ya maboresho ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), yenye wajumbe saba watakaofuatilia kuhakiki madeni ya baraza hilo na kushauri namna ya kuyalipa. Kushoto ni Mwenyekiti wa Tume hiyo, Shehe Issa Omar Issa na Mjumbe, Al Hajj Nuhu Jabir Mruma. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kauli ya Kamanda Muliro yaibua hoja

**Na Mwandishi Wetu**

KAULI ya Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, kwamba raia anaruhusiwa kuomba lifti kwenye gari la polisi, imeibua mjadala huku baadhi wakionyesha hofu ya kubambikwa kesi.

Jumanne ya wiki hii, Kamanda Muliro wakati akihojiwa katika kipindi cha Clouds360 cha Clouds TV, alisema kwa nini mtu asilisimamishe gari la polisi na kuomba lifti.

"Kuna mtu alishawahi kuomba lifti kwenye Defender (gali la polisi) hakupewa? Kwa nini wanapanda watuhumiwa tu? Kwa mfano Defender linakwenda Bunju, Tegeta, Kunduchi, Kitunda au Mwanagati, Kivule analiona kabisa limeandikwa Polisi na wewe unakwenda maeneo hayo kwa nini usilisimamishe ukaomba lift?" alihoji Kamanda Muliro.

Baadhi ya wananchi, wakitoa maoni kuhusu kauli hiyo, walisema kuliko waombe lifti kwenye gari la polisi ni bora waendelee kutembea.

Katika mtandao wa Instagram, Hamisi Mussa aliandika kuwa: "Hawana noma, kweli mimi nimeshapanda toka Mabwepande mpaka Tegeta, kwanza na stori tunapiga vizuri tu."

Amedeus Kiwango aliandika: "Yaani ni bora nikatembea kama ni msituni nikaliwa na Simba kuliko kuomba lifti humo." Mchangiaji mwingine anayejiita Madam ZP aliweka emoji ya kucheka na kuandika, "dah hapana nitatembea tu."

Mchangiaji anayejiita Pi_Tanzania_Official kwa upande wake aliandika, "Naijua iyoo (hiyo) unaingia tu wanakuambia utaenda kutusaidia upelelezi wa 'panya road,' huku Mutta_Ab akiandika kuwa, "Watu wenyewe wanakuangalia kama vile ni washirikina utaanzia wapi?"

**WADAU WAFAFANUA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na Nipashe kuhusu kauli hiyo, alisema si sahihi raia kuomba lifti kwenye magari hayo.

"Si sahihi hata kidogo. Ninadhani aliongea kama kufurahisha umma au kujifurahisha. Gari la polisi ni kama magari ya watumishi wa umma, huwezi kuomba lifti gari la waziri au magereza.

Huo si utaratibu, likitokea tatizo lolote la kibima sheria inakataza kabisa kumpa mtu lifti au kumpandisha mtu ambaye hahusiki," alisema huku akibainisha kuwa magari ya polisi hayana bima kwenye kampuni binafsi, hivyo ikitokea ajali yoyote itakuwa ngumu.

# Samia atua Addis mkutano wa AU

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan jana aliwasili Addis Ababa, Ethiopia kushiriki Mkutano wa 36 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) utakaofanyika kesho na keshokutwa.

Baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Bole jijini humo, Rais Samia alipokewa na ngoma za asili za taifa hilo kisha kukagua gwaride la heshima.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mtandao wa Umoja wa Afrika (AU) pamoja na mambo mengine, mkutano huo utajadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ili kukuza na kuendeleza ustawi na ubora wa maisha ya raia wa Afrika.

Mkutano huo pia utapokea Ripoti ya Marekebisho ya Kitaasisi ya AU itakayowasilishwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame. Pia utajadili Ripoti ya Utawala wa Kisiasa, Kifedha na Nishati Duniani itakayowasilishwa na Rais wa Senegal, Macky Sall.

Nyingine ni Ripoti ya shughuli za Baraza la Amani na Usalama (PSC) na hali ya amani na usalama barani Afrika na Ripoti ya Mgogoro wa Chakula duniani, Ripoti ya Kamati ya Maelekezo ya Wakuu wa Nchi na Serikali (AUDA-NEPAD) na Ripoti ya Kamati ya Kumi ya AU ya wakuu wa nchi na serikali kuhusu Marekebisho ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Miongoni mwa matukio muhimu wakati wa mkutano huo ni uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Afrika (CDC) na uteuzi wa mjumbe mmoja wa Bodi ya Wakaguzi wa Nje wa AU atakayehudumu kwa miaka miwili.

Mwaka jana, mkutano huo ulihudhuriwa na Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango, kwa niaba ya Rais na baadhi ya mambo yaliyojitokeza na kujadiliwa ni kujenga upya uchumi wa Afrika, kuhakikisha amani na usalama wa bara la Afrika, maendeleo ya kijamii na kiuchumi, pamoja na uwakilishi wa Afrika katika taasisi za kimataifa.

Aidha, mkutano huo ulipitisha ombi la Tanzania la kutaka Kiswahili kuwa lugha rasmi ya AU.

# Wadau wapongeza mikopo elimu ufundi

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI serikali ikionyesha nia ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ngazi ya kati kwa ngazi ya astashahada (cheti) na stashahada (diploma), wadau wa elimu wakiwamo walimu, wanafunzi na wazazi wameipongeza hatua hiyo.

Pamoja na kupongeza, wameishauri serikali kuweka mikakati ya namna ya kurejesha mikopo hiyo.

Mwishoni mwa wiki, Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na lile la Zanzibar (ZAHLIFE), alisema serikali inajipanga kufanya hivyo kwa siku zijazo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, mmoja wa wadau hao , Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kimataifa, Utafiti na Ushauri kutoka Chuo cha Bima na Hifadhi ya Jamii Afrika (ACISP), kilichoko jijini Dar es Salaam, Anslemi Anselmi, alisema hatua hiyo ni nzuri kwa kuwa wasomi wa ngazi ya cheti na diploma, ndio rasilimali watu inayohitajika zaidi kwenye uzalishaji.

Alisema kwa nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, wasomi wa ngazi hiyo ni muhimu, akitolea mfano nchi zilizoendelea kama vile China kwamba watendaji na wazalishaji kwenye sekta za viwanda, mabenki na fedha huwatumia hao zaidi.

"Hao ndio tunawahitaji wengi zaidi kwenye uchumi ambao unaochipukia, ukiangalia kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa, ukuaji wa sekta mbalimbali, serikali ikijiwekea malengo ya kukuza pato kwa asilimia 10 tunahitaji nguvu kazi.

"Watu wenye elimu hii wakiwa wa kutosha hata gharama za kazi hazitakuwa juu, kuweka nguvu kuzalisha wataalamu kwa ngazi ya diploma, cheti sisi kama chuo tunaunga mkono, kwa mkakati wa nchi zinazochipukia kama nchi," alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Iringa, Remmy Akarro, alisema kwa kuwa vyuo vya elimu ya juu nchini vinatoa mafunzo kuanzia ngazi ya cheti na diploma, hiyo inaonesha umuhimu wa ngazi hiyo.

"Ukifuatilia vizuri vyuo vyote vikuu, Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Tumaini, Dar es Salaam (TUDARDCo), Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), kuna ngazi ya cheti na diploma. Sasa kwa nini wanafunzi hao wasipate haki, utakuta kuna watoto wanatoka familia maskini sana.

"Utakuta mtoto ana nia na uwezo lakini anashindwa kwa sababu anakosa ada, na watoto wengi, kuna vijana utakuta anaandika barua hataendelea na chuo. Ni uamuzi mzuri sana na kama mwalimu niliyefundisha vyuo vya kati, serikali imecheza kama 'Pele' hapo," alisema.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, kampasi ya Mbeya, Joyce Ibanje, ambaye anasoma ngazi ya cheti katika fani ya ugavi, alisema serikali kuja na hatua hiyo kutasaidia kuwaongezea ujasiri wanafunzi wengi ambao hukwama baadhi ya muhula kutokana na kutokamilisha ada.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo akizungumza kupitia mtandao mmojawapo, alisema kwa sasa Tanzania ina wahandisi kuliko mafundi mchundo, matokeo yake wanaopitia mfumo wa kati ni asilimia 25 na waliobaki wanapitia elimu ya juu.

"Serikali ni vyema kuanza utekelezaji wa mpango wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada nchini," alisema.

**KAULI YA RAIS**

Mwishoni mwa wiki, Rais Samia alisema wanafunzi wa ngazi ya cheti na stashahada kupata mikopo hiyo, alisema jambo hilo halitawezekana kwa sasa lakini watajipanga na kuweka mipango ya kulitekeleza siku zijazo.

"Kwa kazi tunazozifanya sasa hivi na hali ya bajeti, hili bado hatujafikia huko. Kwa hiyo tunalifikiria na tunaliweka kwenye mipango yetu," alisema.

HABARI KITAIFA



Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la Moshi, Pamela Mushi akichukua alama za vidole katika zoezi la kuwafungulia wateja akaunti kupitia huduma ya SimBanking wakati wa promosheni ya kampeni ya 'Benki ni SimBanking' , mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aangua kilio kortini akisomewa mashtaka

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Rhoda Salum (48), jana aliangua kilio mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, huku mikono yake ikitetemeka baada ya kusomewa shitaka lake la kukutwa akisafirisha kilo 23.84 za dawa za kulevya aina ya mirungi.

Baada ya mshtakiwa kutokewa na hali hiyo, Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate alimruhusu kukaa chini huku kesi ikiendelea kwa hatua nyingine.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Caroline Matemu, alidai Januari 26,2023 huko Temeke Wailes, Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akisafirisha kilo 23.84 za mirungi.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo na alirudishwa mahabusu kwa kuwa kiwango cha dawa za kulevya anachoshtakiwa hakina dhamana.

Baada ya mshtakiwa Rhoda kusikia kesi yake hiyo, aliangua kilio huku mikono yake ikitetemeka, ambapo hakimu alimtaka akae chini kutokana na hali yake hiyo.

Mshitakiwa huyo aliendelea kulia hata wakati anatoka kwenye chumba cha mahakama na kurudishwa mahabusu.

Hali hiyo pia ilisababisha ndugu na jamaa waliokuwapo mahakamani hapo nao kulia.

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka, upelelezi katika kesi hiyo umeishakamilika na kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 2, mwaka huu, itakapokuja kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

# Lipumba apata ajali akienda mkutanoni

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amenusurika kifo baada ya gari alilokuwa akisafiria kupinduka katika mazingira ya kutatanisha eneo la Nangurukuru, Kilwa mkoani Lindi.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma wa CUF, Mhandishi Mohamed Ngulangwa, aliiambia Nipashe jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 1:00 usiku wakati kiongozi huyo akiwa ziarani.

"Ni kweli Prof. Lipumba yupo ziarani mkoani Lindi. Baada ya kumaliza mkutano wa hadhara akialikwa kama mgeni rasmi Kinondoni, alialikwa pia mkoa wa Lindi kwa ajili ya kufanya harakati za ujenzi wa chama maeneo mbalimbali," alisema.

Ngulangwa alisema juzi jioni, alikuwa eneo la Njinjo na baada ya kumaliza mkutano wake saa 12:00 jioni aliendelea na safari kwa lengo la kufika Kilwa Kivinje kwa kupitia Nangurukuru.

Alisema baada ya kufika eneo la Nangurukuru, gari lilipinduka na kuharibika vibaya.

"Pamoja na kwamba gari halifai tena, hakuna majeraha mazito waliyopata akiwamo Mwenyekiti Prof. Lipumba. Gari lilikuwa na abiria sita na dereva, jumla wanakuwa saba ambao wote wametoka salama," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema katika msafara huo walikuwamo viongozi wa chama na mwandishi wa habari mmoja.

Kuhusu mazingira ya ajali hiyo, alisema gari hilo limepinduka katika mazingira ambayo kidogo wanayaona ni ya ajabu.

"Gari lilikuwa katika mwendo wa kawaida na sehemu hiyo haikuwa na makorongo. Baada ya kupinduka liliingia mtaroni likiwa tayari limeshageuka chini juu.

Kwa sasa kuna vikao vinaendelea huko kuona namna gani ziara itaen-


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
17 - 02 - 2022

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 18-02-2023 kampuni ya Spedag Interfreight Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Dar es Salaam kupitia Mlandizi gari hizo zina namba za usajili:

**NRB 69149 / NRB152000**

**D500TG-GP / NRB 53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 28.00**
**Upana - mita 4.00**
**Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: Mzenga hadi Dar es Salaam kupitia Mlandizi gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



cotex industries

## TAARIFA KWA UMMA



**JOHN MFUNGO MAJURA**

Hii ni kutaarifu Umma kwamba mwenye picha hapo juu **JOHN MFUNGO MAJURA** si mfanyakazi tena wa **COTEX INDUSTRIES LTD** Mbezi Beach, Jogoo, Dar es salaam kuanzia tarehe 30-09-2022.

Tunaomba kuutangazia Umma kwamba Kampuni ya **COTEX INDUSTRIES LTD** haitahusika na miamala itakayoingizwa au shughuli yoyote itakayofanywa na mtajwa hapo juu kwa niaba ya Kampuni.

**Utawala.**

HABARI KITAIFA

# Kampuni zaunganisha nguvu kujenga uwezo kutoa huduma mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI za usambazaji wa nishati na vilainishi za Engen na Vivo Energy zimeungana na kuwa na uwezo wa kuhifadhi lita bilioni mbili katika nchi mbalimbali za Bara la Afrika ambazo zitasaidia kuongeza upatikanaji wa nishati kwa urahisi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Vivo Energy, Stan Mittelman, alisema jana kuwa kuungana kwao kumefanya wawe na uwezo wa pamoja wa kuwa na vituo vya huduma 3,900.

Alisema nia ya kampuni yake ni kuwekeza zaidi katika kukua kibiashara na kwamba tangu ianzishwe mwaka 2011 wameongeza uwezo wao mara mbili zaidi.

"Miaka minne iliyopita tulinunua soko la Engen katika nchi nane za Afrika na tumeendelea kuhakikisha kwamba, tunakuza na tunakua kibiashara.

"Kumilikiwa kwa Vivo Energy kwa asilimia 100 na Vitol mwaka jana, kulifanya kampuni ikue kwa kasi zaidi. Makubaliano yatakapofikia mwisho katika utekelezaji wa kuunganika kwa Vivo Energy na Engen, tutakuwa tumepiga hatua kubwa zaidi katika soko," alisema.

Kwa mujibu wa Mittelman, Engen ina vituo vya huduma 1,300 katika nchi saba za Afrika na Vivo Energy ina zaidi ya vituo 2,600 katika nchi 23.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mkuu wa Engen, Seelan Naidoo, alisema kuungana kwao na Vivo kunatoa mwanga mpya katika utendaji wa kazi zao na hasa kuendelea kuwa vinara katika soko la Afrika Kusini na mataifa mengine ya Afrika.

Mwenyekiti wa Mwanzilishi Mwenza wa Phembani Group, Phuthuma Nhleko, alisema wanajisikia fahari kuunganika katika ukuaji wa kampuni hizo.

Mwenyekiti wa Vivo Energy, Chris Bake, alisema kwamba kampuni hiyo ina wataalamu na menejimenti imara yenye maono na ubunifu kuwezesha kukua na kuhudumia masoko yake.

# Mahakama yaamuru kutaifishwa ng'ombe

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imeamuru kutaifishwa ng'ombe 71 waliokamatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kuwa mali ya umma.

Aidha, imewatia hatiani watu watano na kuwahukumu kutumikia kifungo cha miezi mitano jela kwa kosa la kuingiza mifugo hifadhini na kuharibu mazingira.

Akisoma hukumu ya kesi namba 13 ya mwaka 2023 jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, alisema wameridhishwa na ushahidi uliotolewa.

Waliohukumiwa adhabu hiyo ni Manekei Hanoti (17), Gwayangwa Hanoti (21), Paulo Ngeresi (24), Shaban Kamaza (26) na Madei Ngahe (23), wote wakazi wa Mwilanja, wilayani hapa.

"Baada ya kusikiliza utetezi wa washtakiwa wote, ambapo mmoja ni mtoto wa miaka 17 pamoja na wenzake ambao hawakuweza kujieleza, mahakama hii imewatia hatiani washtakiwa watano.

"Upande wa mashtaka umefanikiwa kujenga kesi yao kwa kuleta mashahidi wawili na vielelezo, ambavyo ni ng'ombe 68 waliokamatwa na askari wanyamapori wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

"Kwa mamlaka niliyopewa, ng'ombe wote wametaifishwa na ni mali ya serikali. Mahakama hii inaagiza wapigwe mnada kupitia dalali wa mahakama, Kibaigwa Action Mat na fedha za mauzo zilipwe Benki ya NMB kwenye akaunti ya mapato," alisema.

Awali, ilidaiwa na Wakili wa Serikali, Peter Utafu, kwamba Januari 20, mwaka huu, washtakiwa waliingiza ng'ombe hao katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire katika upande wa kijiji cha Sanjaweda.

Wakili Utafu alidai kuwa jambo hilo ni kinyume cha Sheria za Hifadhi za Taifa, Sura 282, Toleo la Mwaka 2002 pamoja na kanuni zake, ikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 351 (1) (a) (b) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Katika hati ya mashtaka, makosa ya washtakiwa ni kuingiza mifugo ya kufugwa nyumbani hifadhini, na kosa jingine ni mifugo kufanya uharibifu wa mazingira kiasi cha kuharibu ikolojia inayowezesha miti kuota upya.

# TAKUKURU yabaini upotevu wa mamilioni stendi ya Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imebaini upotevu wa Sh.380,000 kila siku katika Kituo cha Mabasi cha Nanenane.

Aidha, imesema upotevu huo umetokana na uzembe wa watendaji ikiwamo wananchi kutochukua tiketi mlangoni wakati wa kuingia kituoni. Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema jana jijini hapa kuwa walibaini hayo katika uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko na minada. Alibainisha kuwa kwa mwezi kuna upotevu wa zaidi ya Sh. milioni 11 na kwa mwaka ni Sh. milioni 130, fedha ambazo ni nyingi na zingesaidia kwenye uendeshaji wa shughuli za maendeleo.

Alisema mapato hayo hupotea kutokana uzembe unaofanywa na wakatisha ushuru lakini pia raia wanaoacha tiketi mlangoni ambazo wamekatiwa kwa ajili ya kuingia ndani kutafuta usafiri.

"Suala hili linachangia kwa kiasi kikubwa kupoteza mapato pamoja na ile ya kukaa na fedha za mapato mkononi badala ya kuziweka benki, fedha zinazopotea ni nyingi sana hivyo linapaswa kufuatiliwa kwa kina ili kuokoa upotevu wa fedha hizo katika stendi,"alisema.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE
LABOUR, YOUTH, EMPLOYMENT AND PERSONS WITHDISABILITY
OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH AUTHORITY (OSHA)

OSHA

**Awards for Occupational Safety and Health (AOSH)-2023**

Theme of the year: **A safe and healthy working environment is a fundamental principle and right at work.**




**Introduction**

In commemorating the World Day for Safety and Health at Work and as a part of National OSH promotion and awareness creation activities, Occupational Safety and Health Authority (OSHA) is inviting all owners of workplaces or employers to compete for the Awards for Occupational Safety and Health (AOSH)- 2023.

**Aim**

To encourage private and public workplaces throughout Tanzania to develop, implement and evaluate strategies that help achieve a healthier and safer working environment.

**Entry Eligibility**

Applications are open only for workplaces registered with OSHA and operate in Tanzania Mainland regardless to their affiliation to government, economic sector or financial size are encouraged to participate. More details are found in the Application Platform on our website.

If your workplace has planned or implemented any innovative idea or programme which contributes in the promotion of safety and health at workplace please share with otherstakeholders through this award. All applicants selected for the awards will be visited for verifications.

**Rules for Participation**

i) Visit our website (**www.osha.go.tz**) or directly use this address-(https://wims.osha.go.tz) to create WIMS account or Login if you already have it and complete application as per instructions. You can also apply by filling in a physical form attached in the invitation letter or download it on our website. **Note:** Incomplete applications will not be considered.

ii) Applicant should pay a non-refundable entry fee of TZS 50,000/=. Payments should be done electronically through GePG after being allocated a Control Number.

iii) Award Application is open from an advertisement date until 23rd **April 2023, 15:30 HRS.** Do not attach any document during the submission.

iv) Competitors for AOSH are encouraged to participate in the Occupational Safety and Health Exhibitions to demonstrate their competency.

v) All participants and winners of Awards are invited to attend the award giving ceremony in Morogoro Region on **28th April 2023 or any other date** as may be communicated and they may be asked to be available for media interviews or other publicity.

vi) All written information will be verified by the Award Team. Participants are subject to OSH audits including site audit.

*"Safety and Health at work increase productivity-OSHA can help".*

HABARI KITAIFA

# Malipo ya kahawa yang'oa vigogo KNCU

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TUHUMA za udanganyifu katika mauzo ya kahawa, zimewaweka matatani viongozi watatu wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro (KNCU), baada ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, kuwasimamisha kazi kupisha uchunguzi.

Viongozi hao waliosimamishwa kazi ni Meneja Mkuu wa KNCU, Godfrey Massawe, Meneja Huduma kwa Wakulima, Wilbert Nyela na Mhasibu Wilbard Lyimo.

Kwa pamoja wanatuhumiwa kuuza kahawa kilo 40,283 zilizozalishwa kwa njia ya kilimo hai, mali ya Chama cha Msingi cha Mwika-Kinyamvuo.

Kwa mujibu wa Dk. Ndiege, baada ya kuibuka maswali mengi kuhusu namna uuzaji huo wa kahawa ulivyofanyika tofauti na makubaliano, ameamua kuwasimamisha viongozi hao ili kupisha uchunguzi.

Dk. Ndiege alisema viko vyama 11 ambavyo vinafanya biashara ya kahawa katika Wilaya ya Moshi lakini vinaonekana kuwa na matatizo sawa na chama hicho cha Mwika-Kinyamvuo.

Alisema yako makubaliano ambayo KNCU iliingia na moja ya kampuni kubwa za nje (hakuitaja) kwamba ingenunua kahawa hiyo kilogramu moja kwa Dola za Marekani 4.8.

"Hiyo kampuni ilikubali kununua hiyo kahawa inayotokana na kilimo hai ambayo ukiibadilisha inakuwa kama Sh. 11,000 na zaidi.

Hiyo bei ndiyo wakulima wanasimamia na kweli hiyo taarifa ipo.

"Huyu mnunuzi alitoa Sh. milioni 390 kama malipo ya awali, ndiyo maana maswali yanakuwa mengi. Sasa kama huyu mtu alikubali kuweka hizo fedha inakuwaje anakuja tena anakataa kununua hiyo kahawa? alihoji.

"Ndiyo maana hapa tunasema kuna kitu ambacho sisi hatukijui. Sasa tumeleta timu ifanye uchunguzi halafu tuone. Tumeamua kuwapumzisha ili uchunguzi ufanyike na baada ya uchunguzi majibu yatatoka halafu tutachukua hatua," alisisitiza.

Kabla ya uamuzi huo, inaelezwa kuwa Chama cha Ushirika wa Msingi cha Mwika-Kinyamvuo, kiliingia makubaliano na KNCU kununua kahawa hiyo kwa kilogramu moja inayotokana na kilimo hai kwa Sh. 11,250 baada ya kupata mnunuzi kutoka nje ambaye angenunua kilogramu 40,283 baada kuingia naye mkataba.

Hivi karibuni, Meneja wa chama hicho, Harrison Filex, alisema walichokifanya KNCU kuuza kahawa yao kwa Sh. 4,500 badala ya Sh11, 250 ni nje ya makubaliano na kwamba suala la mnunuzi wa kahawa kutoroka ni jambo la kusikitisha na kwamba taarifa zinazotolewa na KNCU zina ukakasi.

# Kigogo JATU azidi kung'ang'aniwa kuhusu masharti magumu dhamana

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa mashitaka katika kesi inayomkabili Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya JATU PLC, Peter Gasayan, umeiomba mahakama kutupilia mbali ombi la upande wa utetezi la kutaka mahakama kufanya marekebisho ya masharti ya dhamana ili mshtakiwa ayatimize.

Wakili wa Serikali, Caroline Matemu, alitoa ombi hilo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya upande wa mashtaka kujibu hoja za mawakili wa mshtakiwa.

Matemu alidai kuwa hoja ya utetezi kuwa masharti ya dhamana kwa mshtakiwa ni makubwa na kwamba yafanyiwe marekebisho, haina msingi kwa sababu mahakama haiwezi kutengua amri iliyojiwekea.

Wakili huyo alidai kuwa Mahakama ya Kisutu imefungwa mikono na haina mamlaka ya kupitia upya masharti ya dhamana ambayo imeyaweka kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka haki lakini kama hawaridhiki na masharti hayo waende Mahakama Kuu.

Awali, upande wa utetezi ukiongozwa na Wakili Kung'he Wabeya, uliiomba mahakama kupitia upya masharti ya dhamana iliyoyaweka awali na kumpa mteja wao masharti nafuu.

Wabeya alidai kuwa masharti aliyopewa mteja wake ni makubwa na kwamba lengo la kutoa dhamana kwa kuweka kiasi cha pesa au bondi ni kuihakikishia mahakama mshtakiwa afike mahakamani pale anapohitajika.

Wakili Nafikile Mwamboma aliiomba mahakama ipitie upya uamuzi wake kuhusu dhamana ya mshtakiwa na kwamba kabla mshtakiwa hajahukumiwa, ana haki ya kupata dhamana kwa mujibu wa kifungu cha 13 (6) (b) na 15 (1,2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia wakili Mwambona katika maombi yao, aliiomba mahakama iangalie hadhi ya mshtakiwa katika na kuweza hata kumpatia sharti nafuu ikiwemo kusaini bondi.

Kutokana na hoja hizo, Hakimu Mrio aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 27,2023 kwa ajili ya kutoa uamuzi wa suala hilo.

Katika hati ya mashtaka inadaiwa kati ya Januari Mosi na Desemba 31, 2021 mkoani Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia Sh. 5,139,865,733.00 kutoka SACCOS ya JATU kwa madai kuwa angezalisha kiasi hicho cha fedha kwa kuwekeza fedha katika kilimo cha faida wakati akijua si kweli.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

# TAARIFA KWA UMMA

## (Imetolewa chini ya Kifungu na 19 (2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira. Maelezo ya waombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

| S/N | Mwombaji | Anwani | Chanzo cha Maji | Miundombinu | Maelezo ya Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ushirombo | S.L.P 02 Bukombe - Geita. Tanzania. Barua pepe: mdushirombo@maji.go.tz | Visima virefu vinne | Matenki manne yenye uwezo wa jumla ya mita za ujazo 204, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilometa 33.145 pamoja na vilula 14 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Ushirombo |
| 2. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanhuzi | S.L.P 179, Meatu - Simiyu Tanzania Barua Pepe: majimjini@mwanhuziuwssa.go.tz | Maji ya bwawa lililopo Mwanahinya | Matenki ya maji manne yenye jumla ya mita za ujazo 640, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 61.97, pamoja na vilula 35 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Mwanhuzi |
| 3. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa | S.L.P 185, Maswa. Barua Pepe: info@maswawssa.go.tz | Maji ya bwawa lililopo Zanzui na visima virefu 7 | Matenki ya maji matatu yenye jumla ya mita za ujazo 1,100, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 343 pamoja na vilula 105 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Maswa, Malampaka, Lalago |
| 4. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi | S.L.P 64, Bariadi. Barua Pepe: mdbariadi@maji.go.tz | Visima virefu 27 | Matenki ya maji 14 yenye jumla ya ujazo wa mita za ujazo 1,840, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 175, pamoja na vilula 79 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Bariadi |
| 5. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kasulu | S.L.P 9, Kasulu - Kigoma. Barua Pepe: mdkasulu@maji.go.tz | Vyanzo vya chemchemi 2 vilivyopo Nyanka na Nyakatoke pamoja na Mito miwili ya Miseno na Chai | Matenki ya maji 4 yenye jumla ya ujazo wa mita za ujazo 552, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 67.8, pamoja na vilula 10 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Kasulu |
| 6. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo | S.L.P 22, Namtumbo-Ruvuma | Mto Matogoro uliopo Kijiji cha Libango na Mto Rwinga | Matenki ya maji 6 yenye jumla ya mita za ujazo 615, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 112 na hakuna vilula. | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Namtumbo. |
| 7. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makete | S.L.P 6,Makete Njombe | Vyanzo vitatu vya maji ambavyo ni mito ya Ivalalila na Kidwiva na chemchem ya Ludihani | Matenki ya maji 6 yenye jumla ya mita za ujazo 573, mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 128 na hakuna vilula. | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Makete |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi

**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz**
**Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kasi utoaji elimu ya bima iongezwe ili kuokoa wengi

**SEKTA** ya bima ni muhimu katika maisha ya kila siku na kwa kadri zinavyosonga mbele, baadhi ya watu wameanza kupata mwamko wa kutambua umuhimu wake. Hali hiyo imewafanya wengi kutambua umuhimu wanapopata majanga mbalimbali mfano kama mali haikuwa na bima, wanaishia kupata hasara huku aliyekuwa nayo akipata fidia.

Athari za kutokuwa na bima ni kubwa kuliko za kuwa nayo ndiyo maana baadhi ya watu hukata bima mapema, huku nchi zilizoendelea ikiwa ni lazima kuwa na bima kwa kuwa jambo lolote linaweza kutokea.

Mfumo wa bima unavyofanya kazi unalipa kiasi cha fedha kilichokadiriwa kabla ya huduma. Kama ni afya mtu analipa na siku unapokwenda hospitalini kwa ajili ya matibabu, anahudumiwa yeye na wategemezi wake bila kuulizwa kiasi cha fedha.

Wako ambao hawaamini kwenye bima kwa kuwa wameishi kwa miaka mingi kwenye nyumba wanazomiliki lakini hawajakutana na janga la moto. Kwa vyombo vya moto pia ni lazima kuwa na bima ili kusaidia mtu anapopata ajali au chombo kuungua.

Kwa maana halisi, bima ni mkataba wa biashara kati ya mtu mmoja, au kikundi cha watu, taasisi au shirika, ili mradi kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria. Bima kazi yake kubwa ni kuchukua jukumu la kutoa ahadi ya kulipa hasara itakayotokana na uharibifu wa mali, upotevu wa mali na kifo.

Kuna aina nyingi za bima kama bima ya ajali za barabarani, bima za moto, bima za mafuriko, bima za kimbunga, bima za afya, bima za maisha na nyinginezo. Licha ya kuwapo kwa bima za aina mbalimbali, ndani ya jamii bado uelewa kuhusu bima ni mdogo, hivyo kusababisha kundi kubwa la Watanzania waliofanya uamuzi wa kuwa nazo kutoridhisha.

Miongoni mwa sababu zinazotajwa sana kwa nini mwamko uko chini ni ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu bima na hiyo imesababisha watu wengi kutokujua umuhimu wake katika dunia ya leo. Pamoja na wengi kuelewa umuhimu wa bima, wako baadhi wamekuwa wakipuuza kutumia fursa hiyo kukatia kinga mali zao vikiwamo vyombo vya usafiri. Lakini pindi wanapokumbwa na majanga kama vile kuunguliwa na nyumba na mali kuteketea au ajali ya gari na chombo hicho kuharibika kwa asilimia kubwa, wanajikuta wakiingia katika majuto.


Ukweli haupingiki kuwa kukata bima kunahitaji kuwa na fedha na ni gharama kiasi lakini kwa kuangalia faida zake kwa mahitaji ya mbeleni kama janga linaweza kutokea, ni wazi ni jambo mtambuka kulifanya.

Bima ni mkataba wenye taswira mbili kwa upande mmoja unaofanana na aina nyingine za mikataba kama ilivyo kwa mkataba wa watu wawili kuuziana mali kuingia ubia, ili kushirikiana katika kuendesha biashara. Lengo huwa ni kumnusuru yule aliyekata asipate hasara na kuyumba pindi anapopata matatizo ama majanga yasiyotarajiwa kumtokea.

Kutokana na hali hiyo diyo maana kuna taasisi nyingi ikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), ili wananchi waelewe na kuona umuhimu wa kukata bima kwenye mali na maisha yao, ni vyema elimu ya kutosha kuhusu kinga ya majanga na uhakika wa huduma, kwa maana ya bima ikatolewa.

Lakini kwa hali halisi ya sasa, ni muhimu kila Mtanzania akawa na bima ya afya, mali na maisha ambazo kwa kiasi kikubwa zitasaidia kupooza machungu pale mtu anapokutwa na janga liwalo lote. Pia kampuni za bima yanatakiwa kutumia njia ambazo ni rahisi kuwafikishia wateja wao na kuwafahamisha huduma na mambo mengine muhimu ya bima, ikiwa ni pamoja na uhakika wa kuondoa ubabaishaji na udanganyifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Suala la migogoro wafugaji na wakulima liangaliwe kwa kina

Na Halfani Chusi

**SUALA** la wafugaji na wakulima, kuuwana na kupeana majeraha limekuwa kitu cha kawaida, jambo ambalo kama halitafanyiwa utatuzi wenyetija linaweza kupelekea kutokea kwa maafa makubwa nchini.

Mara nyingi kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wakulima wakiwatuhumu wafugaji kwa kuingiza mifugo kwenye mashamba yao hali ambayo hupelekea kuzuka kwa mtafaruku mkubwa dhidi yao.

Inaporejewa, matukio ya kikatili miezi mitatu iliyopita huko Mkoani Pwani Wilaya ya Kibaha kulitokea tukio la kijana aliye shambuliwa hadi kuvunjwa mkono na wafugaji wa jamii ya kisukuma wakati alipokuwa akijaribu kuwazuia wasiingize mifugo kwenye shamba lake.

Hata hivyo, polisi mkoani humo ilichukua hatua ya kudhibiti ikiwa ni pamoja na kuwahamisha wafugaji waliokuwa karibu na mashamba ya wakulima.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo kupitia sakata hilo, akaagiza mtuhumiwa aliyetenda kosa hilo akamatwe na afikishwe kituo cha polisi kwa ajili ya hatua za kisheria.

"Kwenye kupambana na hali hiyo, tulishafika mpaka sehemu yenye migogoro, tukaamuru wafugaji waondoke eneo lile kwa sababu licha ya mifugo kuharibu mazao ya wakulima lakini bado ilikuwa inachangia kuharibu miundombinu na vyanzo vya maji" alisema.

Licha ya kuwapo kwa malalamiko hayo, bado kumeendelea kuripotiwa kwa matukio ya kinyama wanayofanyiana makundi hayo, hapo ndipo dhana ya kuwekeza nguvu kwenye utatuzi wa madhila hayo inapohitajika.

Mnamo Februari 2 mwaka huu, gazeti hili liliripoti wafugaji walivyouwa maofisa misitu kwa kutumia panga na shoka, kwenye msitu wa hifadhi ya kijiji cha Chakulu na Ilunde wilayani Uvinza, mkoani Kigoma.

Ni kitendo kilicholaaniwa vikali na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kupitia Mkurugenzi wake Ana Henga, akitaka serikali kufanya uchunguzi wa kina kuhakikisha waliohusika na kutenda kosa hilo wanachukuliwa hatua za kisheria.

Ni hali inayotishia amani kutokana na muendelezo wa matukio hayo, ambayo wafugaji wamekuwa wakiyafanya pale wanapohitaji sehemu za malisho kinguvu, ipo haja ya mamlaka husika kukaa chini na kutafakari kwa kina lini migogoro kati ya wafugaji na wakulima itafikia ukomo.

Kama imefikia hatua hadi askari anauliwa vipi kwa raia wa kawaida? Ni dhahiri kuna kitu hakipo sawa kati ya wafugaji na wakulima, jambo linalohitaji utatuzi wa kina.

Undani wa hilo kama Nipashe ilivyothubutu kudodosa, unaonyesha kuna wakati wafugaji wanakuwa wakorofi kwa wakulima, lakini wakati mwingine wakulima wanakuwa wakorofi kwa wafugaji. Hiyo mara huishia na sintofahamu kati ya sehemu ya malisho na kilimo.

Mkulima mwingine wa mahindi kijijini Msagali, katika wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, akasema mara nyingi hulazimika kulala shambani kulinda mifugo kama Ng'ombe na Mbuzi, isiingie shambani kula mazao.

"Ninalala shambani kwa sababu, nisipofanya hivyo wafugaji wanaweza kuingiza mifugo yao, nikakosa chochote kama ilivyokuwa mwaka jana.

"Mwaka jana niliikuta mifugo imetawala shamba langu ikabidi niwatafute wahusika lakini nilipowapata walikuwa wabishi kulipa mpaka kesi ilipofika mahakamani" Kibago anasimulia kilichomsibu.

Pia, mkulima wa mkoani Iringa, wilaya ya Kilolo, katika kata ya Nyanzwa, naye ana kilio sawa na mtangulizi wake, akiiomba serikali kuangalia namna ya kumaliza migogoro ya kila siku kati ya wafugaji na wakulima.

"Watu wanapigana, wanapeana ulemavu wa kudumu, wengine wanakufa kisa migogoro ya wafugaji na wakulima, hili si jambo la kufumbiwa macho, watu wanapoteza maisha" analalamika.

# Bidhaa za Kioo za kwanza soko la AfCFTA

**Na Joseph Mwendapole**

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, ameishauri kampuni ya Kioo Limited kuendelea kuzalisha bidhaa za kioo kwa wingi na zenye ubora na viwango vinavyohitajika katika Soko la Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA).

Aidha, amekishauri Kiwanda hicho kuzalisha bidhaa za kioo zitakazotumika kama vifungashio kwa wajasiriamali wadogo ili kuhimili ushindani katika biashara na kuingia AfCFTA.

Dk. Kijaji aliyasema hayo juzi alipotembelea kiwanda hicho kilichoko Chang'ombe, Dar es Salaam, kwa lengo la kuangalia bidhaa zinazozalishwa na zinazotarajiwa kuingizwa katika soko hilo.

Pia alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nane za mwanzo zilizopewa kipaumbele cha kupeleka bidhaa kwenye soko hilo na miongoni mwa bidhaa 10 zitakazotangulia kuingia katika soko hilo kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, ni pamoja na kahawa, marumaru na kioo.

Mkurugenzi wa Kiwanda hicho ambaye aliomba jina lake lisitajwe, alisema Kiwanda cha Kioo kiko tayari kuingiza bidhaa ya kioo katika soko la AfCFTA kwa kuwa kina uwezo wa kuzalisha zaidi ya chupa milioni moja kwa siku ambazo huuzwa ndani na nje ya nchi.

Pia alisema kiwanda hicho kinatengeneza kioo kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini kama mchanga, chokaa, 'feldspar' na soda 'ash' kutoka nje ya nchi kwa sasa.

Kadhalika, alisema asilimia 40 ya chupa hizo hutengenezwa na mabaki ya chupa zilizotumika hivyo amewaomba wananchi kukusanya kwa wingi mabaki ya chupa zilizotumika ili kurahisisha upatikanaji wa malighafi ya uzalishaji wa chupa hizo na kutunza mazingira.

Alisema kampuni hiyo iko tayari kuunga mkono juhudi zozote zinazofanywa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika Tanzania, Adam Mihayo alipotembelea makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Mihayo, alimhakikishia mkuu huyo, kuwa benki yake itaendelea kutoa ushirikiano katika shughuli za kikanda za kiuchumi na za uwezeshaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni kuimarisha upatikanaji haki yazinduliwa

**Na Elizabeth Zaya**

WIZARA ya Katiba na Sheria, imezindua kampeni ya Kitaifa ya huduma ya msaada wa kisheria yenye jina la Mama Samia inayolenga kuimarisha upatikanaji haki, itakayofanyika nchi nzima katika vijiji na vitongoji kwa miaka mitatu mfululizo.

Akizungumza wakati akizindua kampeni hiyo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema wameamua kuzindua kampeni hiyo ili kutatua matatizo mengi ambayo bado yanaikabili sekta ya upatikanaji haki nchini.

Alisema kampeni hiyo itashirikiana na taasisi zote za kisheria za serikali na za binafsi za Tanzania Bara na Zanzibar zilizosajiliwa katika kufanya kazi hiyo nchi nzima.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo wamepanga kwenda kuyashughulikia ni pamoja na utoaji wa elimu kwa wananchi namna ya upatikanaji wa haki za binadamu na sheria mbalimbali zinazotekeleza haki za binadamu.

Lingine, alisema ni elimu kuhusu haki ya ukatili wa kijinsia ambalo alisema bado kuna kazi kubwa ya kufanya kutokana na kuendelea kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini.

"Na hivi karibuni tumeshuhudia kuongezeka kwa vitendo hivi nchini, kwa hiyo tunaamini kwamba kampeni hii itasaidia kwa kiwango kikubwa," alisema.

Lingine ni la mirathi pamoja na migogoro ya ardhi, maeneo ambayo alisema kumekuwa na matatizo makubwa.

"Eneo hili la mirathi bado tunasumbuka sana, nalo lina ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, kwa hiyo tunakwenda kuelimisha wananchi juu ya mifumo ya kisheria, tutajenga pia uwezo kwa taasisi na mtu mmoja mmoja katika eneo hili. Kwa mfano bado tuna zile mila ambazo zinazuia wanawake wasimiliki wala kurithi mali,"alisema Dk. Ndumbaro.

"Katika kampeni hii tutahakikisha elimu ya kutosha inatolewa ili kuhakikisha kila mtu akiwamo mwanamke anarithi na kumiliki mali na ardhi," aliongeza.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Geofrey Pinda, alisema kila mwaka watakuwa wanafanya tathmini kujua matokeo ya kampeni hiyo na kuziomba taasisi zote zinazoshughulikia utoaji haki kushirikiana kufanikisha hilo.

Mtaalamu Mbobezi wa Masuala ya Ulinzi wa Watoto wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Victoria Mgonela, alisema kampeni hiyo itasaidia kwa kiwango kikubwa kutatua matatizo yanayosababishwa na kukosa ufahamu wa kisheria.

Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini Tazania (RITA), Lina Msanga, alisema katika kutekeleza majukumu yao, wamekuwa wakikutana na mambo mbalimbali ya migogoro na kwamba kampeni hiyo itakua msaada kwao na watashiriki kufanikisha.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Kamishna wa Mafuta na Gesi, Michael Mjinja (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua mafunzo katika chuo cha Veta mkoa wa Tanga juzi, kwa ajili ya Watanzania 170 ya kusimamia usalama, uhifadhi wa mazingara na afya za wafanyakazi wa mradi wa bomba la mafuta (EACOP), linalojengwa kutoka Hoima Uganda mpaka kijiji cha Chongoleani mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yapongeza Watanzania 170 kupatiwa mafunzo bomba la mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeusifu mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kwa kuwapatia mafunzo yenye hadhi ya kimataifa Watanzania 170 kwa ajili ya kuanza ujenzi unaotarajiwa kuanza kati kati ya mwezi huu.

Maeneo hayo waliyopatiwa mafunzo Watanzania hao ni katika kusimamia afya, usalama wa wafanyakazi wakiwa kazini na utunzaji wa mazingira katika maeneo yote yanayohusu mradi.

Bomba hilo la mafuta linajumlisha eneo lenye kilomita 1,443 kutoka Kabaale, Hoima nchini Uganda hadi katika kijiji cha Chongoleani kilichoko Tanga.

Akizungumza wakati wa kuzindua mafunzo hayo ya kuwaongezea ujuzi na maarifa Watanzania 20 kati ya walengwa 170 ambao bado wengine wanaendelea na mafunzo katika Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Tanga na Arusha, Kamishna wa Mafuta na Gesi kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Micheal Mjinja, alisema Watanzania hao watakuwa rasilimali muhimu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa na serikali ili kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mjinja aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni pamoja na ule wa gesi asilia (LNG) ambao uchimbaji wake utafanyika chini ya ardhi na baharini.

"Mradi huu una manufaa makubwa kwa taifa. Mbali na biashara ya mafuta, ajira nyingi zinatengezwa na wataalam wazawa kuzalishwa kwa ajili ya miradi mingine ya kimkakati," alisema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Uwezeshaji Watu wa EACOP, Martha Makoi, alisema katika utekelezaji wa mradi huu, kila mkandarasi ana kipengele kinachomtaka kuwapa mafunzo wafanyakazi wazawa katika jinsi zote (kike na kiume) ili kuzalisha wataalamu na kuwajengea uwezo.

Alisema ndiyo maana Watanzania 170 watapewa mafunzo hayo na tayari 20 kati ya hao wamehitimu katika chuo cha VETA mkoani Tanga, huku wengine 25 wakiendelea na mafunzo yao katika chuo cha Arusha.

Mmoja wa wahitimu hao, Sabrina Salim, mwenye Shahada ya Mazingira aliyoipata kabla ya kupewa mafunzo haya, alisema kauli mbiu yao wakati wa mafunzo na itakayotumika katika eneo la mradi ni 'Usalama Kwanza'.

Martha Joash Makenge kutoka kampuni ya Daqing Oilfield Construction Group iliyopewa kazi ya ukandarasi wa kujenga matangi na sehemu za kuhifadhia mafuta, mafunzo haya hutolewa kwa ushirikiano na chuo cha VETA cha Moshi na Arusha na hutambulika kimataifa.

Alisema kuelekea utekelezaji wa mradi huo, tayari kazi ya awali , ikiwemo kusafisha maeneo mradi utakakopita na kuwalipa wananchi wanaopitiwa na zoezi hilo la ujenzi wa bomba la mafuta lenye urefu wa kilomita 1443 kutoka Kabaale, Hoima nchini Uganda mpaka Chongoleani mkoani Tanga.

Asiadi Mrutu, kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) naye alisema maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa bomba, ambalo limegusa ajira za zaidi ya Watanzania 1672 yamekamilika.

Alisema jumla ya watu 9508 watalipwa fidia kwa kupitiwa na mradi huo, ambapo 8922 (zaidi ya asilimia 93) wamekubali kupokea fidia hiyo na tayari watu 8450 wameshalipwa kiasi cha shilingi bilioni 29 za Kitanzania kama fidia na kupewa notisi za kuhama maeneo yao ifikapo mwezi Mei mwaka huu ili kupisha ujenzi.

Julien Bouwense, Meneja wa Bandari ya Mafuta inayojengwa katika kijijini cha Chongoleani, alisema ni matumaini yake kuwa Watanzania na Waganda watafurahia zaidi matunda ya mradi huo pindi utakapokamilika.

Neema Mwakatobe, Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi kutoka Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ameusifu mradi wa EACOP kwa kuwapatia Watanzania mafunzo hayo muhimu kupitia mradi huu mkubwa wa kimkakati.

# Madaktari bingwa moyo kukutana Dar

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), imeandaa mkutano wa kimataifa wa shambulio la moyo utakaofanyika kwa mara ya kwanza nchini kuanzia leo jijini Dar es Salaam.

Wakati ikitangaza mkutano huo, taasisi hiyo imewaasa wananchi kuwahi hospitali wanapoona dalili za shambulio la moyo, kwa kuwa wakichelewa zaidi ya saa moja ni rahisi sana kufariki.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo.

Alisema walengwa wa mkutano huo wa siku mbili ni madaktari bingwa wabobezi, madaktari bingwa, madaktari, wateknolojia wa moyo, wanafunzi wa udaktari pamoja na wauguzi wanaotoa huduma za dharura. Dk. Kisenge alisema kauli mbiu ya mkutano huo ni "Shambulio la moyo ni hatari kwa maisha yako, wahi hospitali".

Alisema katika mkutano huo kutakuwa na watoa mada kutoka ndani na nje ya nchi ambao watafundisha jinsi ya kuwahudumia wagonjwa wanaopata tatizo la shambulio la moyo.

Dk. Kisenge alisema wataalamu hao wataelezea umuhimu wa wagonjwa hao, kuwahi mapema hospitali mara tu wanapopata matatizo hayo.

"Dalili za shambulio la moyo ni kupata maumivu ya kifua upande wa kushoto, kifua kubana, kushindwa kupumua na wakati mwingine maumivu ya tumbo,"alisema.

Alisema tatizo la shambulio la moyo linachangia vifo vingi duniani na ndiyo sababu JKCI imeamua kutoa kipaumbele kwa elimu ya shambulio la moyo.

"Tatizo ni kubwa na ukiangalia kuna vijana hata wa miaka 35 wanapata shambulio la moyo kwa hiyo wataalamu kutoka Marekani, Agentina, Misri, India, watatoa mada mbalimbali wakishirikiana na madaktari bingwa wa hapa nchini," alisema.

Alisema serikali ya awamu ya sita imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye taasisi hiyo ambao umeiwezesha kuwa na mashine kubwa mbili ambazo zimegharimu Sh.bilioni 11.

Aidha, Dk Kisenge alisema Oktoba mwaka 2022 JKCI ilianzisha huduma ya matibabu ya maumivu ya kifua ambapo mgonjwa mwenye tatizo hilo aliyekuwa akifika kwenye kliniki alipata huduma ya dharura inayotolewa kwa saa 24.Alisema tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo wamefanikiwa kuwaona wagonjwa 38 ambao walipata tatizo la shambulio la moyo na kufanikiwa kuokoa maisha yao.

"Mgonjwa anayepata shambulio la moyo anatakiwa kupata matibabu ndani ya saa moja na iwapo atachelewa kupata matibabu anaweza kupoteza maisha. Niwasihi wananchi mnapopata dalili za shambulio la moyo wawahi hospitali mapema kwaajili ya matibabu," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mafunzo wa JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, alisema magonjwa ya shambulio la moyo ndiyo yanaongoza duniani kwa vifo.

Alisema inakadiriwa kwamba watu zaidi ya milioni 2 wanapata shambulio la moyo (heart attack), kila mwaka na silimia kubwa wanafariki dunia.

Alisema tamwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa watu wengi wanaopoteza maisha kwa shambulio la moyo wanatoka nchi za kusini mwa jangwa la Sahara Tanzania ikiwemo.

Alisema magonjwa hayo yanasababishwa na vitu mbalimbali ikiwemo shinikizo la damu, uvutaji wa sigara, kisukari, ulaji usiofaa na kunywa pombe kusiko kwa kawaida.

"JKCI haiwezi kupigana vitaa hii peke yake lazima tushirikishe mataifa mengine tubadilishane uzoefu wa namna ya kushughulikia matatizo kama haya na ndiyo sababu tumeitisha mkutano huu," alisema Pallangyo.



# H'shauri Hai kupata mamilioni usajili taxi, bajaji, bodaboda

**Na Godfrey Mushi,** HAI

ADA mpya ya usajili wa huduma za magari madogo ya kukodi mjini maarufu kama taxi, bajaji na pikipiki za abiria (bodaboda), zitainufaisha Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, zaidi ya Sh.milioni 6.485 mwaka ujao wa fedha.

Kingine ni ushuru wa maegesho ya magari ambayo nayo yatainufaisha Sh. milioni tatu, wakati ushuru wa kuegesha bajaji utaipa Sh.milioni nne.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka, alisema makusanyo hayo yamo katika makisio ya mapato yatakayokusanywa mwaka 2023/2024.

Alikuwa akizungumzia vyanzo hivyo vya mapato ya ndani katika mkutano wa Baraza Maalum la Madiwani, lililoketi kupitisha mapendekezo ya mpango na bajeti ya halmashauri hiyo inayotarajiwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 43.3.

"Tukaweke nguvu katika makusanyo ya mapato ili kuisaidia halmashauri yetu kufikia malengo yake ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

"Tuna mapendekezo ya maombi maalum ya shilingi bilioni 16.9 kwa ajili ya kuombewa fedha nje ya bajeti kutoka serikali kuu, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 30 ya shule za msingi, ujenzi wa nyumba 20 za shule za msingi na ujenzi wa madarasa 15 ya shule za sekondari.

"Ukarabati wa maabara 36 za shule za sekondari, ujenzi wa Soko la kwa Sadala, ujenzi wa jengo la utawala, ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi, ununuzi wa gari la Mkurugenzi, ununuzi wa gari la Halmashauri na ujenzi wa matundu ya vyoo shule 20 za msingi."

Aidha, Rutaraka, alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuwasukuma watendaji wa idara ya mpato, kuhakikisha wanapeleka mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) katika masoko mapya ya Maiputa na Gezaulole ili kuisaidia Halmashauri hiyo kufikia malengo yake ya kukusanya mapato.



Balozi wa wa Utalii wa Tanzania nchini Marekani, Macon Dunnagan (kushoto), akiwa na baadhi ya wapanda mlima wenzake kutoka katika nchi hiyo, katika eneo la Simba Camp jana, wakati wakiwa katika safari yao ya siku sita ya kuupanda mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika. **PICHA: JAMES LANKA**

## LATRA yaweka mtego mabasi yanayopandisha nauli kiholela

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewawekea mtego wasafirishaji wa abiria wanaotoa huduma kati ya Sanya Juu na West Kilimanjaro hadi Bomang'ombe, Wilaya ya Hai, baada ya kuibuka malalamiko ya kupandisha nauli kiholela.

Wanaotuhumiwa kupandisha nauli kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 3,000 ni wasafirishaji wa daladala aina ya noah na hiace.

Akitoa ufafanuzi jana kuhusu malalamiko hayo ya abiria, Ofisa Mfawidhi wa LATRA, Mkoa wa Kilimanjaro, Paul Nyello, alisema ingawa bado hawajapata malalamiko rasmi, wanafuatilia kwa karibu uhalali wa kupandishwa nauli hiyo.

Kuzidisha nauli kinyume na nauli elekezi ni kosa kwa mujibu wa LATRA, na ukibainika faini yake ni Sh. 250,000.

"Tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo. Nakumbuka walishalalamika kipindi cha nyuma kupitia Mkuu wa Wilaya aliyepita (Thomas Apson).

"Niwatoe wasiwasi wananchi kwamba LATRA, inalifanyia kazi na sheria itachukua mkondo wake. Tutafanya doria ya kushtukiza ili kuona ukweli wa malalamiko haya, hasa ya kuzidisha nauli, kukatisha safari na kufanya biashara ya kusafirisha abiria bila ya kuwa na kibali,"alisema ofisa huyo

Kutokana na malalakimo hayo, baadhi ya wananchi wamesema hawakubaliani na ongezeko hilo la nauli na wanaitaka LATRA kusitisha mara moja kwa kuwa kuiacha ni kuumiza wananchi.

"Hawa jamaa wamepandisha nauli, tumelalamika sehemu mbalimbali, ikiwamo kwa madiwani, lakini malalamiko yetu ni hewa hayasikilizwi,"alisema Zakaria Mmari.

Alisema daladala hizo kibaya zaidi hasa noah zinabeba abiria badala ya wanane, wanabeba 16 mpaka kwenye buti.

Elizabeth Jonh alisema nauli kuanzia Sanya Juu kwenda West Kilimanjaro, wanatozwa kuanzia Sh.1,500, Sh. 2,000 hadi Sh. 3,000.

# Wawili kortini tuhuma kukutwa na nyama ya pundamilia

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Ngolay, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, wameburuzwa kortini wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, baada ya kushtakiwa kwa makosa ya kukutwa wakimiliki vipande viwili vya nyama mbichi ya pundamilia.

Washtakiwa hao waliofikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Babati kujibu tuhuma hizo, mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Jumaa Mwambago ni Mosuru John (50) na Mary Mtambo (50).

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Blandina Msawa, alidai kuwa Januari 21 mwaka huu, washtakiwa walikutwa na nyama hiyo, ambayo ni sawa na mnyama mmoja aliyeuwawa mwenye thamani ya Sh. milioni 2.850.


Kwa mujibu wa Msawa, washtakiwa hao walikiuka kifungu cha 86 (1) (2) (b) cha Sheria ya Wanyamapori, Sura ya 283 ya Mwaka 2002.

Baada ya kusomwa hati hiyo, Hakimu Mwambago, alisema kwa kuwa kesi hiyo ni ya uhujumu uchumi, mahakama hiyo haina uwezo wa kuisikiliza, ila imepewa kibali cha kuanza kuisikiliza.

Alipomaliza kauli hiyo, Hakimu Mwambago aliwahoji washtakiwa kila mmoja kama shtaka alilosomewa ni kweli, ambapo wote walikana.

Hakimu Mwambago alisema dhamana dhidi ya washtakiwa iko wazi na kila mmoja anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tatu, barua ya utambulisho wa mali isiyohamishika, kitambulisho cha taifa au cha kupigia kura na awe mkazi wa Babati.

Kutokana na masharti hayo, washtakiwa wote walikosa wadhamini, hivyo Hakimu huyo kuamuru kwenda mahabusu hadi Februari 28 mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.





## Daladala zatishia kusitisha huduma kisa uwapo wa bajaji

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAMILIKI wa daladala mkoani Mwanza wametishia kugoma kutoa huduma ya usafiri katika Jiji endapo bajaji zitaendelea kufanya biashara ya kubeba abiria.

Walitoa malalamiko hayo juzi jijini Mwanza mbele ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA), Habib Suluo alipokutana na viongozi wa bajaji, pikipiki, madereva wa daladala pamoja na wamiliki wa magari hayo.

Walisema bajaji zinatakiwa kukaa katika vituo maalum kwa ajili ya kusubiri abiria lakini siyo kuingia barabarani na kusimama katika vituo vya daladala na kuanza kupakia abiria kwa Sh. 500 ama 1,000.

Walisema bajaji katika Jiji la Mwanza zinawasababishia biashara zao kuwa ngumu kwa sababu na wao wanasafirisha abiria badala ya kukaa vituoni ili wakodiwe.

Mwenyekiti wa madereva wa daladala mkoani Mwanza, Mjarifu Kezirahabi, alisema vyombo vimesajiliwa kwa mujibu wa sheria na kupangiwa kazi za kufanya.

Alisema daladala zimesajiliwa kusafirisha abiria mkoani Mwanza na bajaji pia zimesajiliwa maalum kwa ajili ya kutoa huduma ya kukodiwa na siyo kufanya safari za kupakia na kushusha kama yalivyo magari.

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habib u Suluhu, alipiga marufuku bajaji kubeba abiria katika vituo vya daladala mkoani Mwanza.

Alisema bajaji zimesajiliwa kukaa vituoni ili zikodiwe na siyo kujigeuza kuwa daladala na kuanza kubeba abiria kwa kuwapandishia na kushusha kwenye vituo vya daladala.

Aliongeza kuwa kila chombo kilisajiliwa kwa mujibu wa sheria na kwamba kinatakiwa kufanya kazi kama kinavyoelekezwa na sheria za nchi na siyo vinginevyo. Mkurugenzi wa Huduma za Uchukuzi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Aron Kisaka alisema lengo la kukutana na wadau hao ni kukukumbushana majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Aliwataka madereva wa daladala na bajaji kuzingatia sheria ili kila mtu aweze kufanya kazi yake aliyopangiwa kufanya.

Alisema bajaji kwa mujibu wa sheria hazipaswi kujigeuza kuwa daladala na kuanza kupakia abiria badala yake zinatakiwa kukaa katika vituo na kusubiri kukodiwa.

Baada ya mvutano mkali wa wadau hao, madereva wa bajaji walikubali kufanya kazi zao kama usajili unavyowataka kwa kukaa vituoni na kusubiri wakodiwe na siyo kupakia abiria kama zinavyofanya daladala.

# Mke wa Mwenyekiti aliyefariki kwa madai kubakwa azikwa

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

MWILI wa aliyekuwa mke wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa National Housing Kata ya Rwamishenye Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Khadija Ismail anayedaiwa kubakwa na kisha kuuawa kwa kupigwa na kitu butu kichwani umezikwa.

Akitoa neno la pole kwa familia hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Erasto Sima baada ya mwili huo kukabidhiwa kwa ndugu wa marehemu alitoa pole kwa wafiwa, huku akisema mtuhukiwa aliyefanya mauaji hayo bado anatafutwa.

"Tunaendelea kutoa pole kwa familia, ndugu jamaa na marafiki wa marehemu tangu jana lilipotokea tukio hili na tumeendelea kuchukua hatua zile za uchunguzi, mpaka kuruhusu familia wachukue mwili.

"Ni kwamba mambo ya serikali yameshakamilika japokuwa bado kijana huyo hajapatikana tuendelee kutoa ushirikiano sisi kama wananchi kwa yeyote atakayepata taarifa za kijana huyu alipo atoe taarifa kwa mamlaka husika," alisema Sima.

Aidha, aliwasihi wananchi wa Mkoa wa Kagera kutoa taarifa za wageni kwa wenyeviti wa mitaa ili kusaidia kubaini wahalifu.

Mume wa marehemu, David Dominick aliwashukuru wananchi pamoja na viongozi kwa ushirikiano walioutoa kwa familia, huku akiwaomba kuendelea kuwatia faraja katika kipindi hiki kigumu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Willium Mwampagale tukio hilo lilitokea baada ya mtuhumiwa Paschal Kagwa (22) aliyekuwa amepewa hifadhi na familia hiyo kumuua mke wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na kisha kumbaka.



Baadhi ya Wahandisi kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, wakila kiapo cha utii mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa wa Mwanza, Monica Ndyekobora (hayupo pichani), baada ya kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), jijini Mwanza juzi. **PICHA: ROSE JACOB**

# MaRC, maofisa elimu wapewa siku saba kuwasaka wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKUU wa wilaya na maofisa elimu mkoani Shinyanga wamepewa wiki moja kuhakikisha wanafunzi 2,344 wa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni wawe wameripoti.

Pia Jeshi la Polisi limeagizwa kukamilisha upelelezi dhidi ya watuhumiwa ambao wamewapa ujauzito wanafunzi.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yahaya Nawanda alitoa maagizo hayo juzi kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Nawanda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, alisema hajaridhishwa na mwenendo wa wanafunzi kuripoti shule mwaka huu.

Wanafunzi 2,344 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu mkoani Shinyanga mpaka sasa bado hawajaripoti kuanza masomo.

"Wakuu wa wilaya, maofisa elimu na watendaji wote wa serikali natoa wiki moja tu hadi kufika siku ya jumatano, nipewe taarifa kuwa wanafunzi 2,344 ambao bado hawajaripoti shule kuanza kidato cha kwanza wawe darasani hata kama hawana sare za shule," alisema Dk. Nawanda.

Aliongeza: "Kama mnaona itakuwa ngumu niambieni ili niingie mwenyewe mitaani kuwasaka hawa wanafunzi, ila naamini mtaweza lakini kama ikishindikana naingia mwenyewe.

"Tunataka wanafunzi wote wapate elimu na kutimiza ndoto zao kama adhima ya Rais Samia inavyotaka ndiyo maana amekuwa akitoa fedha nyingi kujenga miundombinu ya elimu" alisema.

Pia aliliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kuhakikisha wanakamilisha upelelezi wa kesi za mimba za wanafunzi, ili watuhumiwa wafikishwe mahakamani na kuchukuliwa hatua kali za kisheria na kuwa fundisho kwa watu wengine kuacha kufanya mapenzi na wanafunzi.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako akiwasilisha taarifa ya elimu kwenye kikao hicho, alitaja takwimu za wanafunzi ambao wamepewa ujauzito na kuacha masomo mwaka jana kuwa ni 147 kati ya hao 28 ni kutoka shule za msingi na 119 sekondari.

Alifafanua kuwa kati ya wanafunzi 28 wa shule za msingi ambao walipewa ujauzito, kesi ambazo zipo mahakamani ni mbili, 26 bado upelelezi haujakamilika.

Alisema mimba 119 za sekondari kesi 21 ndiyo zilepelekwa mahakamani, tatu zilitolewa hukumu 22 zinaendelea kusikiliza, na kesi 38 bado upelelezi wake haujakamilika.




## Marufuku isiishie kwenye vitabu





# BUFE

IJUMAA FEBRUARI 17, 2023 BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe


## Naibu Waziri afunguka uwekezaji kitaifa kupitia TEHAMA ' sasa hodi hospitalini'

# Benki ya Dunia yamwagia sifa Samia kuvuka vilivyowashida wengi Afrika

**Na Peter Orwa**




Rais Dk., Samia Suluhu Hassan, alipofanya mazungumzo na Rais wa Benki ya Dunia, David Malpass, katika makao makuu ya, benki hiyo Washington DC, nchini Marekani. **PICHA:MTANDAO.**

HIVI karibuni Benki ya Dunia imetoa ripoti ambayo imekuwa na sura kuu mbili, ikiibebesha sifa Tanzania kiuchumi.

Eneo la kwanza, inaishangaa namna Tanzania ilivyohimili misukosuko ya uchumi duniani, hali kadhalika ikitoa baadhi ya majibu ya siasa ya uchumi kitaifa yanayohojiwa nchini, kwa baadhi ya mambo yanayoshika uchumi nchini.

Toleo hilo la wiki hii linaloitwa Ripoti ya Kiuchumi ya Tanzania; Upatikanaji wa Majisafi kwa Maisha Bora na Umuhimu wa Kupatikana Mfumo wa Maisha Bora, ina ufafanuzi namna Tanzania ilivyomudu magumu ya kiuchumi kimataifa, kuanzia mwaka 2021.

Kimsingi, ni kipindi tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani, dunia ikiwa katika misukosuko mingi, ikiwamo janga la ugonjwa Covid - 19, mahsusi ripoti ikielekeza angalizo kwa nchi za Kusini mwa Janga la Sahara.

Ripoti hiyo inafafanua kwamba wakati nchi jirani na Tanzania barani Afrika, uchumi wake ukishuka kwa wastani asilimia mbili za pato lao la taifa, hali ilikuwa kinyume Tanzania ikishuhudiwa uchumi wake unapanda kwa wastani wa asilimia mbili.

Hapo kuna juhudi za kiongozi mkuu wa nchi kupandisha uchumi wa nchi zimeushangaza utafiti wa Benki ya Dunia, hadi mwishoni mwa mwaka huo 2021 penye misukosuko, uchumi wa Tanzania ukaongezeka kufika wastani asilimia 4.3 na mwaka unaofuata 4.8, ilhali kukiwapo makadirio kufika mwaka huu, wastani huo utapanda kufika asilimia 5.3.

Benki ya Dunia inarejea hata penye mlipuko wa maradhi UVIKO-19 barani Afrika, baadaye kukutwa na vita baina ya Russia na Ukraine, inayotikisa uchumi wa dunia yote, Tanzania bado imekuwa katika nafasi nzuri barani Afrika.

Itakumbukwa hata athari za mlipko wa maradhi Uviko 19, umekuwa wa chini sana, kulinganisha na ilivyo kwa hata baadhi ya nchi jirani katika Afrika Mashariki.

Benki ya Dunia, inasifu hatua za serikali nchini katika ufanisi kwenye uchumi, biashara na huduma, mahsusi ikitaja maboresho katika shughuli za utalii, kufunguliwa mipaka ya biashara na mafanikio kwenye chanjo dhidi ya UVIKO 19, hata nchi haikuathirika sana.

Katika mbinu zake kukuza uchumi, Rais Dk. Samia mara baada ya kuingia madarakani, Machi 2021, alifanya ziara za kibiashara zinazofungua tija na milango ya biashara kitaifa katika nchi jirani na mbali, sasa zikitajwa kuwa na tija kubwa ka uchumi na biashara nchini.

Ziara jirani zenye tija kubwa katika biashara ya nchi, zinajumuisha katika mataifa kama; Kenya, Uganda, Malawi na Rwanda.

Itakumbukwa, katika Sekta ya Utalii, Rais Dk. Samia katika moja ya mikakati yake ya mwanzo kukuza Sekta ya Utalii, alishiriki sinema ya Royal Tour, ambayo inaonyesha mapinduzi makubwa katika sekta hiyo ya Utalii.

Sekta ya Utalii, ni moja ya maeneo makubwa katika mchango kwa uchumi wa taifa, ajira, na kuingiza fedha za kigeni.

Benki ya Dunia, katika ripoti yake hiyo inayozama kwenye maisha bora, kupitia huduma za maji na nyendo bora za kiuchumi, inafafanua kwamba kuwapo na misingi imara ya kiuchumi, ndiyo imekuwa siri kuu ya mafanikio ya nchi.

Hata kurejea hoja za ukinzani kisiasa unajitokeza, ikiwamo bungeni kuhusu kasi ya kupanda kwa bei ya vyakula na bidhaa za kilimo, Benki ya Dunia, imerejea ilichokiita 'vikwazo vya nje'.

Katika hilo, ripoti hiyo ya wiki hii inajumuisha kudorora kwa kilimo kunakotokana na ukame ulioikumba nchi, kupanda bei ya mafuta ya petroli kimataifa, kulikosababisha usafiri wa shida na kupanda bei za vyakula.

Itakumbukwa, serikali ilishatoa ufafanuzi, ikianza na kilimo katika msimu uliopo ambao uko katika hatua ya mavuno, ikishauri wakulima kupanda mazao yanayohimili ukame katika msimu uliopo, kutokana na hali mbaya ya hewa.

Pia, baada ya kuwapo vita baina ya Ukraine na Russia, mara moja bei ya mafuta ilipanda kimataifa na hatua nchini ikalazimika kupandishwa bei ya petroli kulikotangazwa na serikali.

**MFUMUKO WA BEI**

Ni siku chache tu zimepita serikali ilitangaza kuwapo kasi ya mfumuko wa bei, chakula kikitajwa chanzo kikuu, hata kuchukuliwa hatua na serikali ya kukaribisha tani 90,000 za mchele kutoka nje, ili kukabili makali hayo ya bei.

Hata hivyo inaporejewa sura ya pili ya ripoti hiyo kimataifa, Benki ya Dunia inauweka kwenye uzani wa kundi la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kwamba ina nafuu kubwa.

Kutokana na misukosuko ya kiuchumi, nchi wanachama wa SADC zina mfumuko wa bei kiwango cha asilimia 10, ikitolewa mfano wa taifa la Zimbabwe, ambako kunatajwa ni wastani wa mara mbili na nusu zaidi kwa hali iliyoko nchini

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

# Naibu Waziri afunguka uwekezaji kitaifa kupitia TEHAMA ‘ sasa hodi hospitalini’

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeendelea kuwekeza katika Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, kwa lengo la kutatua changamoto ya mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuvutia uwekezaji na kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Huduma za mawasiliano ni za msingi katika maisha ya wananchi kwa vile zinagusa nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia, mawasiliano yanawezesha kuhimili sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, kilimo, uwekezaji, biashara na ajira.

Maeneo mengine ni benki na utalii, ambako kunaongezewa ufanisi wa kiutendaji sambamba na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa moja kwa moja kupitia sekta hizo.

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew, ametamka hayo akiwa katika ziara yake ya kukagua miradi ya mawasiliano, ubora na upatikanaji wa huduma za mawasiliano, na usikivu wa redio na uhakiki wa anwani za makazi wilayani Mafia, Pwani.

Anasema Wizara yake inabeba miundombinu yote ya mawasiliano nchini na sasa imeongezewa bajeti, kuakisi uhalisia wa kazi adhimu inayotakiwa kufanyika katika masuala ya



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Kundo Mathew.

TEHAMA nchini.

“ Bajeti ya wizara hii ilikuwa Sh.bilioni nane kwa mwaka lakini Rais Samia alivyoingia madarakani aliipatia Sh.bilioni 230,” anasema Kundo na kuongeza:

“Shilingi bilioni 230 maana yake ni miradi mingi zaidi ya ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano, ajira za moja kwa moja na miundombinu inapoimarika zaidi huduma za mawasiliano zinazidi kupatikana kwa urahisi na gharama zake zitaendelea kuwa nafuu.”

Kundo anasema, katika jitihada zinazofanywa na serikali katika uwekezaji ni kwenye miundombinu ya TEHAMA, katika bajeti ya mwaka 2022/23 serikali imetoa Sh.bilioni 145 kwa ajili ya ujenzi wa mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Anasema, hadi sasa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umeunganishwa na nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo(DRC), ili kusaidia kutoa huduma pamoja na maeneo mengine ya mpakani.

Pia, anaongeza kuwa, mnamo Juni 26, 2021, serikali kupitia aliyekuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima, ilizindua Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Awamu wa Tano katika mkutano ulioshirikisha wadau wa sekta hiyo, alieleza mpango mkakati umejielekeza kuleta matokeo katika maeneo matano ya kimkakati.

Anataja malengo hayo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa kuendelea kujenga miundombinu, kuongeza watumishi, vifaa tiba, dawa na vitendanishi, kuimarisha utayari wa kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na dharura kwa kuboresha mfumo wa kutoa taarifa ya viashiria hatarishi, ushirikishwaji wa jamii, usafi wa mazingira.

Pamoja na udhibiti wa taka hatarishi, upatikanaji wa fedha, mabadiliko chanya ya tabia na ushirikishwaji wa sekta nyingine.

Eneo jingine ambalo serikali imejielekeza ni kuendelea na jitihada za kuboresha kitita cha huduma za afya katika ngazi ya msingi na huduma za rufaa, huduma za utengamano, huduma shufaa,za tiba asili na tiba mbadala.

**MIKAKATI TEHAMA**

Kuhusu utekelezaji wa mikakati hiyo ya TEHAMA katika Sekta ya Afya, Mratibu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) Kanda ya Pwani, Baraka Eliezer anasema kuwa mfuko huo unatekeleza mradi muhimu wa tiba mtandao, inayogusa hospitali katika mtandao mmoja.

Anasema, dhamira ni kuhakikisha hospitali zenye huduma bora zaidi zinasaidia zile ambazo hazina wataalamu wa kutibu magonjwa bobezi na vifaa vya kisasa kwa njia ya mtandao, bila kumlazimu daktari aliyekuwapo kwenye hospitali za taifa za rufaa kwenda kwenye hospitali za mikoa au wilaya.

Anasema hivi karibuni serikali imetumia takribani Sh.bilioni mbili kujenga miundombinu ya kuziunganisha hospitali za mikoa na za rufani, kiwa ni azma yake ya kuboresha sekta ya afya nchini kwa kutumia TEHAMA.

“Kupitia TEHAMA daktari bingwa mbobezi wa kutibu masuala ya neva kutoka Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) anaweza kutoa huduma katika hospitali zilizopo mikoani bila mgonjwa kusafirishwa kwenda MOI, Dar es Salaam. Mradi huu tulianza kuutekeleza miaka miwili iliyopita na tuliona hili ni eneo muhimu sana na linaenda sambamba na lengo letu la kuhakikisha jamii inanufaika na TEHAMA,”anasema Eliezer.

Aidha, Mhandisi huyo ameishukuru serikali ya sasa, kuhakikisha kwamba UCSAF inaendelea kupata fedha zinazowezesha kuwa na miundombinu ya Tiba Mtandao katika hospitali mbalimbali nchini.

Katika upande wa Zanzibar, Eliezer anasema tayari serikali kupitia UCSAF inatekeleza mradi mkubwa wa Tiba Mtandao ili kutatua changamoto za kutoa huduma za kibingwa kwa kuziunganisha Hospitali za Abdallah Mzee iliyopo Pemba na Mnazi Mmoja iliyopo Unguja, pamoja na Hospitali za MOI na Jakaya Kikwete za Dar es Salaam .

Anasema, mradi huo unategemewa kukamilika kabla ya mwezi Juni mwaka huu na kwamba kukamilika kwake kutasaidia kuleta mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya kwa upande wa Zanzibar.

Naibu Waziri anasema kuwa, mfumo wa afya uliopo sasa unailazimu serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutumia gharama kubwa kwa mgonjwa anapotoka Zanzibar kwenda kupata huduma za rufaa Tanzania Bara na hivyo UCSAF itahakikisha huduma zote za rufaa zinapatikana pia katika Hospitali hizo za Abdallah Mzee na Mnazi Mmoja zilizopo Zanzibar.



Maonyesho ya Teknohama yakiendelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Benki ya Dunia yamwagia sifa Samia kuvuka vilivyowashida wengi Afrika

**INATOKA UK 11**

(asilimia 240).

Hata kwenye maeneo ya kisekta ambayo yanaiwezesha Tanzania kuangukia nafuu ya kiuchumi na kupata sifa, imo eneo la vyakula kukitajwa kuwapo maboresho makubwa.

Katika mpango wa taifa na bajeti ya kilimo mwaka huu, Rais Dk. Samia akafanya mageuzi makubwa zaidi, kukiwapo bajeti ya kilimo ikielekezwa Sh. 751,123,280,000 katika mwaka uliopo wa fedha, kutoka Sh. 294, 162,071,000 za mwaka wa fedha uliotangulia, 2021/23 sawa na ongezeko la asilimia 255.

Kwa mujibu wa mapedekezo yaliyowasilishwa na kupitishwa bungeni, yanajumuisha wakulima kupata ruzuku ya mbolea na kuendelezwa kwa skimu mbalimbali za umwagiliaji, kupisha janga la ukame kwenye kilimo na uhaba wa mazao.

Pia, Rais Dk. Samia ni hivi karibuni akiwa jijini Dakar Senegal kuhudhuria kikao cha maendeleo ya Afrika, ambako aliwasilisha mada na ajenda mojawapo muhimu ikiwa kilimo, alifanya faragha na baadhi ya wawekezaji kimataifa, kuanzisha viwanda vya mbolea nchini, kukiendana na kupata majibu chanya.

Ripoti ya Benki ya Dunia inataja maeneo yaliyofanya vizuri kuinua utawala wa Rais Dk. Samia, yanajumuisha pia maeneo ya huduma za bima, makazi, sekta za fedha na teknolojia ya mawasiliano.

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, eneo lingine la mapato ambalo linaonyesha mabadiliko ya uchumi kukua katika zama za Serikali ya Awamu ya Sita, inaangazia kwenye mapato yasiyo ya kodi.

Hapo inafafanua kwamba, katika mwaka wa fedha 2020/ 21 ilikuwa wastani wa asilimia 2/1, lakini yakapanda hadi kuwa asilimia 2.7 katika mwaka wa fedha uliofuata, 2021/22.

**MAUZO YA NJE**

Tangu aingie madarakani mwaka 2021, Rais Dk. Samia, mauzo ya bidhaa zilizozalishwa nchini zilifanya vizuri, nusu yake zikitokana na bidhaa migodini.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, bidhaa zilizozalishwa ambazo huchukua asilimia 20 ya bidhaa zote, mauzo yake yalipanda kwa asilimia 36 katika mwaka wa fedha 2021/22 kutoka asilimia 36 za mwaka wa fedha 2020/21, ikiwa na ishara zote za ukuaji maradufu. Huduma za utalii nazo zikafanya makubwa nchini, kukaribisha pato la taifa na fedha za kigeni.



TAFAKURI YA MLALAHOI

# Marufuku isiishie kwenye vitabu, pia kwenye nyimbo na maandiko






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

MIAKA ya nyuma tukiwa shule ya msingi, siku moja tukiwa darasani, aliingia mgeni wakati mwalimu akifundisha. Na si kama kawaida, kwa nidhamu tukasimama na kumsalimia: “Shikamoo mwalimu!”.

Hiyo ilitokana na nidhamu tuliyokuwa tumejengewa na walimu wetu, kuwa ukiona mtu mzima anakuzidi umri mwamkie shikamoo na akiingia darasani aamkiwe shikamoo, lakini kwa kuwa tuliamini kila anayeingia ni mwalimu, tukamwamkia kwa kumtambulisha kuwa mwalimu.

Tulipokwisha mwamkia, alipita moja kwa moja akaenda kwenye madawati ya nyuma na mwanafunzi mmoja akampisha na kusogea mbele yeye akakaa mahali pake. Kwa kawaida wanafunzi walioketi karibu naye waliingiwa na hofu.

Hivyo, siku hiyo hata sisi tuliingiwa wasiwasi hata tuliokaa mbele kila mara tuligeuka kumwangalia mgeni wetu alikuwa pale kwa jambo gani. Lakini, muda wote alionekana akiandika kitu huku akifuatilia mwalimu wetu alichokuwa akifanya.

Kipindi kilipomalizika, ndipo mwalimu akamtambulisha mgeni kwetu, kuwa ni Mkaguzi Elimu, ametoka Ofisi ya Elimu ya Wilaya. Wageni hao waliendelea kuja kila mara, kwa mtindo uleule na baadaye tukawazoea.

Kumbe wakati huo, wakaguzi hao walikuwa na tija sana, wakifuatilia nini kinafundishwa kwa wanafunzi, uwezo wa walimu na hata wanafunzi wenyewe, miundombinu ya kufundishia na kujifunza kama inastahili na inatosha.

Hatimaye, wakaguzi hao waliandika taarifa za ukaguzi wao na kuziwasilisha kunakohusika kwa waliowatuma na kama kulikuwa na changamoto zilifanyiwa kazi na mambo yaliendelea. Elimu ilikuwa juu kutokana na uwajibikaji huo.

Siku za baadaye, utaratibu huo ulidorora kama si kutoweka kabisa na hivyo walimu na wanafunzi kufundishana walivyojua wao, bila hata kukaguliwa, pengine kutokana na ongezeko la shule, lakini na viongozi waliofuatia kutoona umuhimu wa ukaguzi.

Kukosekana ukaguzi, kumefanya sasa kila mtu ‘lwake’, kuna shule zikawa na mitaala yake, vifaa vyake na walimu wa aina yake waliyotaka wao. Zikaanzishwa shule za kimataifa zenye mitaala ya Kiingereza, zikitafuta walimu zilizowataka wa kufundisha kwa Kiingereza.

Kila shule ikaingiza vitabu vyake kutoka ilikojua, ili mradi itimize lengo lake la kufundisha watoto na kufaulisha na kujiendesha kibiashara, kwamba shule iliyofaulisha ndiyo iliyopata wanafunzi wengi hivyo ada na malipo mengine kuongeza kipato.

Kutokana na kukosekana kwa ukaguzi shuleni, katika shule za umma na binafsi, hivi karibuni vitabu vya kila aina viliagizwa kutoka nje, vingine vikitoka kwa wafadhili na matokeo yake kumbe ni vya kupotosha watoto.

Ni vitabu vinavyoenda kinyume na maadili, utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, vikifundisha watoto mambo yasiyostahili kwa umri wao, vikiwafundisha jinsi ya kujamiiana, tena kwa maandishi na michoro.

Hatimaye, serikali ikabaini uovu huo na mara moja kutangaza kufungia vitabu 16 vilivyokuwa vikitumika shuleni kufundishia, vyote vikiwa na uchafu huo uliokithiri, usioendana na utamaduni wa Mtanzania.

Najiuliza, ilikuwaje mpaka vitabu hivyo vikatumika shuleni na walimu wakiona vinafaa kufundishia katika mazingira na muktadha wa taifa hili? Hakuna aliyeona ukakasi, hata kuendelea kufundisha kana kwamba hana watoto nyumbani?

Pengine, waliofanya hivyo walipofushwa na fedha, wamiliki wa shule walipofushwa na mapato yatokanayo na ada, huku walimu wakipofushwa na mishahara waipatayo. Je, serikali ilikuwa wapi muda wote huo? Kwanini shule hazikaguliwi? Ni uzembe tu! Serikali kupitia wizara yenye dhamana ya elimu, inapaswa kutimiza wajibu wake wa kusimamia shule bila kujali ni za umma au binafsi,kwani wasomao humo ni Watanzania wenye utamaduni,mila na imani za Kitanzania. Wasiachwe kama kuku wa kienyeji kuchakura elimu na kupokea yoyote.

Sasa basi, hili funzo tulilopata kwenye vitabu litumike, pia kwenye maudhui ya vyombo vyetu vya habari kwa maana ya magazeti, redio, runinga, mitandao ya kijamii, pia nyimbo za wasanii, ambako nako kuna uchafu mwingi unarushwa, kuandikwa na kuimbwa.

Tuangalie sana tamthiliya, maigizo, vichekesho, katuni na hata nyimbo zetu zinazoimbwa na hao tunaoamini kuwa wasanii nguli nchini, tunaowaogopa na wengine kuwatumia kwenye kampeni zetu. Kuna nyimbo hazipaswi kuachwa zikaendelea kusikilizwa na watoto! Alamsiki!

BIASHARA

# Kifurushi aina yake, mteja wa pikipiki anadhaminiwa na bima afya ya bure

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kanuni za utumishi wa umma, serikali inasisitiza hoja ya usalama mahali pa kazi. Hiyo ni kutokana na kubaini hatari zinazojitokeza kwenye maeneo hayo ya uzalishaji bidhaa huduma, pia ni umma unakosaka riziki.

Hapo ndiko kunajitokeza kundi la watumishi wa bodaboda, linatajwa hali si salama sana kazini mwao, ikiwamo kipengele cha kujikimu pindi wanapopatwa na tatizo.

Matatizo yenyewe ni kama vile kuumwa, au ajali zinazowapata mara nyingi. Ni kawaida kumkuta mwendesha bodaboda anahangaika pesa ya matibabu kwa ajali inayompata, ikizingarwa na wengi wao bado wako mbali na huduma ya bima ya afya.

Cha kujiuliza, inakuwaje wengi wao hawajikimu na akiba ya kujihami na majanga kama hayo? Jibu lao kuu wakiamini 'nitapata kesho'.

Hapo ndipo serikali kupitia Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, inaamua kuingilia kati na majibu, ya Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, ikitarajiwa kupuguza madhara kesho kwa umma.

Hapo ndipo kuna kampuni ya kuuza pikipiki aina TVS, imeibua kifurushi cha kuwawezesha wateja wake kujikimu, pindi wanapopata majanga na madhara kama kifo na ulemavu wa kudumu

Ni huduma inayotolewa bure, sharti ni mteja anayenunua pikipiki kwenye kampuni, anakuwa ameshajiunga kiasi kinachofikia shilingi milioni tano.



Meneja wa Mauzo wa Kanda, Razack Kasanga, akitoa elimu kwa baadhi ya bodaboda wanufaika wa TVS kuhusu utunzaji pikipiki hizo, pamoja na kifurushi cha bima. **PICHA; HALFANI CHUSI**

Meneja wa Mauzo Kanda ya Dar es Salaam, Razack Kasanga anafafanua: "Jambo jingine ambalo kampuni ya TVS hufanya kwa wateja wake ni kuwapa huduma ya bima ndogo ya mwaka mmoja, usajili bure, waranti ya mwaka mmoja, pia tumeweka kifurushi cha Rider Cover kwa kila mteja atakayenunua pikipiki ya TVS."

Kwa mujibu wa Razack, mteja anapopata ajali kubwa, hata kushindwa kuendelea na udereva au kupoteza maisha, basi yeye au familia yake hupata fidia hadi Sh. Milioni Tano, inayoitwa Rider Cover, kwa sharti ajali iwe imethibitishwa polisi, pia kuwa na leseni ya udereva.

**KWANINI HUDUMA HIYO?**

Kasanga, anasema wameongeza huduma hiyo, walipogundua waendesha bodaboda wengi wakipata ajali, wanashindwa kumudu gharama za matibabu, hata kuangukia kwenye madhara.

"Akipewa (shilingi) milioni tano, anaweza kufanya biashara nyingine na kujikwamua kiuchumi tofauti na bodaboda au kununua pikipiki nyingine na kumkabidhi mtu mwingine, awe anaendelea kumletea fedha hata akiwa katika hali ambayo hawezi tena kufanya kazi" anasema Kasanga.

**BODABODA WAFUNGUKA**

Nipashe ilipita kwenye vituo vya bodaboda kupata maoni ya madereva wahusika, wengi wakisifu huduma ni ya kipekee na imewagusa nafsi zao.

Dereva bodaboda maeneo ya Kigamboni Mji Mwema, Ashuni Kilemile, ambaye mbali na kuzimwagia sifa pikipiki TVS kwa kubana mafuta ikisafiri kilomita 65 kwa lita, nguvu ya kubeba mzigo na kupanda mlima na lita moja.

Anafafanua: "Hiyo ni huduma muhimu, sasa inaonyesha ni kwa jinsi gani kampuni zinazojihusisha na biashara ya kuuza pikipiki, zimeanza kuja na ubunifu wa kutujali sisi watumiaji.

"Kama TVS wana kifurushi ambacho mtu akipata matatizo anaweza kupewa hadi milioni tano, kitu ambacho kipindi cha nyuma hakikuwepo kwa hiyo kwa muktadha huo unaona ni kwa jinsi gani huduma hiyo ilivyo na mantiki."

Mwendesha bodaboda mwingine wa Mabibo, Dar es Salama, Jackob Kilamba, anaeleza: "Hapo awali ilikuwa rahisi sana kuibiwa pikipiki, hata ikiwa imepaki, mwizi alikuwa na uwezo wa kuwasha pikipiki hata bila kutumia ufunguo.

"Lakini, kwa teknolojia ya sasa, kwenye pikipiki za TVS, hatoweza kuondoka na pikipiki hadi mmiliki husika airuhusu kuwaka kwa kifaa maalumu kama rimoti.

"Hii teknolojia imekomesha wezi wote waliokuwa wanaiba pikipiki na kuwasha kwa kuunganisha waya bila kutumia ufunguo," anasema.

Saidi Winsley, bodaboda wa kituo cha Kawe, Dar es Salaam, anasema kifitishi hicho kipya kimemshawishi kununua pikipiki aina hiyo ya kipekee na kinara hivi sasa.

"Lengo nifanye kazi bila shaka yoyote, kwa sababu ukiangalia gharama ya kukata bima tu yenyewe ni kubwa sasa kama ukinunua pikipiki kutoka kwenye kampuni yao unapata ofa hiyo kwa nini usichangamkie fursa?," anasema Saidi

# Unajua kulikoni majina ya kampuni yanaishia Limited?

**Na Joran Herman**

NENO 'Limited' au 'Ltd' linajulikana mara nyingi, likifuata jina la kampuni fulani, mfano Mbuguye Company Limited (Ltd).

Pia, kuna mazoea ya neno 'Plc', likifuata jina la kampuni tajwa. Inawezekana mtu anasoma au anaendelea kusoma, bila ya kupata ufahamu namna maneno hayo yanaandikwa mbele ya majina ya kila kampuni nchini.

Kisheria, kuna kampuni za aina mbili; binafsi, pia za umma. Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002, inazitaka kampuni binafsi kuwa na neno 'Limited(Ltd)kama sehemu ya jina lake.

Zile za umma, zinahitaji neno 'Public Company Limited' (Plc), ikiwa sehemu ya jina lake. Hivyo, mtu anapoona jina la kampuni fulani atambue ni binafsi,vilevile penye neno 'Plc' inakuwa la umma.

Pia, kuna tofauti kisheria kati ya kampuni binafsi na ya umma. Mojawapo ni vyanzo muhimu vya mitaji yao.

Kwa ile binafsi, inakuwa na hisa(shares) kulingana na uhitaji wa kampuni na kuuzwa kwa watu, ambao baada ya kuzinunua hukabidhiwa cheti cha umiliki wake na wanaitwa wanahisa.

Kampuni ya umma, yenyewe inatangaza hisa zake kwenye soko la hisa la Dar es Salaam (DSE)na upande wa kampuni za umma, zinatangaza kuuza hisa zake kwa wana kampuni tu.

Katika kampuni binafsi, mwanahisa anakuwa mmiliki wa kampuni,kwa maana anakuwa na haki kuhudhuria vikao na kutoa uamuzi mkubwa, huku nguvu zake zinasimama kulingana na asilimia za hisa zake kwenye kampuni. Kadri zinavyokuwa hisa nyingi,ndiyo kunakuwapo sauti zaidi. Kampuni hutangaza hisa na zinanunuliwa kwa kuzilipia moja kwa moja, au malipo ya baadaye. Hilo la baadaye, hufanyika ama kampuni itakapozihesabu au kuhitaji hisa hizo kulipwa. Kitaalamu inaitwa 'paid and unpaid shares'.

Mfano mojawapo ni kwa mwanahisa anayenunua hisa 1000, kisha analipia hisa 500 na zinabaki 500. Baadaye kampuni inaweza kumhitaji mwanahisa alipie hisa 100,ambazo hakuzilipia awali(called shares)na hisa 400 zilizobaki zitaitwa-uncalled shares, kwa maana ya hisa ambazo kampuni bado haijazihesabu au bado haijahitaji zilipwe.

Neno 'Limited' au 'Limited Liability' ni kampuni yenye dhima ya ukomo. Maana yake ni kwamba, taasisi hiyo inajitegemea dhidi ya wanahisa.

Hapo inabeba maana kwamba kampuni hiyo inaweza kushtaki, pia wanahisa hawawezi kushitaki au kushtakiwa. Kampuni inawajibika peke yake kwa jina lake, pindi yanapotokea madai kwa kampuni inapofilisika na inatakiwa kufungwa.

Katika hilo wanahisa hawawajibiki kwa madeni ya kampuni. Wadai wa kampuni iliyofilisika, hawawezi kuwashtaki wanahisa kwa madeni ya kampuni yao. Hapa ndipo kwenye nafasi ya neno 'Limited' linaposimama.

Daima wanahisa hawawezi kushitakiwa, kwa sababu kampuni yao imeshindwa kulipa madeni au mali zao binafsi, haziwezi kukamatwa kwa sababu yoyote ya kushindwa kulipa madeni, isipokuwa watawajibika kisheria kulipa hisa walizokuwa hawajazilipa awali (unpaid shares) au hisa ambazo kampuni ilikuwa haijazihesabu au haijahitaji zilipwe (uncalled shares).

Kwa hiyo wajibu wao kisheria una ukomo au unakoma kwenye hisa ambazo walikuwa

hawajazilipa au hisa ambazo zilikuwa hazijahesabiwa na kampuni. Wanahisa hawawajibiki kisheria kutumia mali zao binafsi, kulipa madeni ya kampuni.

Neno 'Limited' katikia kampuni inayotoa ulinzi kisheria kwa wamiliki wa kampuni dhidi ya madeni yake, pale inapotangazwa kufilisika. Kampuni ndiyo itawajibika dhidi ya madeni na sio wamiliki wa kampuni.

**Mwandishi wa makala hii ni mwanasheria na wakili wa mahakama.**



# Wizara ya Habari, TSA waingia makubaliano ya ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Kampuni ya Tanzania Startups Association (TSA) zimesaini makubaliano ya ushirikiano wa kuanzisha na kuimarisha miongozo mbalimbali inayosimamia ubunifu na kampuni changa nchini.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo juzi jijini hapa, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dk. Jim Yonazi, alisema lengo ni kuhakikisha kampuni changa na bunifu zinakuwa na mazingira bora ya kiutendaji pamoja na kulifikia soko la bidhaa wanazozalisha.

"Tunaenda kutengeneza mazingira bora ya kisera na kisheria ili kuhakikisha yale yanayofanywa na kampuni changa (startup) yanachagiza mipango ya kitaifa ya maendeleo na kushiriki kukuza uchumi wa nchi,"alisema.

Aidha, alisema mikakati iliyopo ni kuhakikisha TEHAMA inakuwa nguzo muhimu kwa vijana kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha kampuni changa na bunifu mbalimbali na kutatua tatizo la ajira pamoja na kuzifikia fursa za masoko zilizopo ndani na nje ya nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya TSA, Zahoro Muhaji, alisema kampuni hiyo inamilikiwa na wanachama na ipo kama mwamvuli wa startups zote nchini.

Alisema kuwa kampuni changa na bunifu mbalimbali zitakuwa na manufaa zaidi katika nyakati zijazo kwa kuzingatia kwamba asilimia kubwa zinatumia TEHAMA hivyo zitachangia kukuza uchumi wa kidijiti.

"Kuna uwezekano mkubwa wa kampuni changa yaani startups kuchangia kukuza pato la Taifa na kutengeneza ajira wa wastani wa ajira 70 kwa kila startups,"alisema.

Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Mifumo ya TEHAMA wa Wizara hiyo, Mulembwa Munaku alisema kuwa makubaliano hayo yanaenda kufungua fursa kwa vijana kusaidiwa zaidi katika bunifu zao na kuchochea ajira kwa kutumia TEHAMA.

# Wamiliki malori watoa mapendekezo vyanzo vya mapato

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI serikali ikiwa kwenye maandalizi ya bajeti ya mwaka 2023/24, wamiliki na wasafirishaji wa malori wametoa mapendekezo ya vyanzo vya mapato huku wakiomba kupunguzwa kwa kodi wanayotakiwa kuilipa kabla hawajapata faida.

Kodi hiyo katika mwaka wa fedha 2022/23 inatozwa Sh.milioni 2.7 kwa kila lori moja jambo ambalo limesababisha baadhi ya wamiliki kushindwa kulipa na kupendekeza iwe Sh.milioni moja kwa mwaka ili wafanyabiashara wasikimbie kusajili magari hayo nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa baada ya kuwasilisha mapendekezo ya Chama cha Wamiliki wa Maroli Wadogo na wa Kati (TAMSTOA) na Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT) kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mwenyekiti wa wamiliki hao, Chuki Shabani, alisema wamewasilisha kwa serikali bajeti mbadala ya kodi hiyo kutokana na iliyopo hailipiki.

Alifafanua kuwa kodi hiyo awali ilikuwa inalipwa Sh.800,000 na baadhi ya wasafirishaji walishindwa kulipa kodi hiyo na matokeo yake walinyang'anywa na serikali na ilipopanda hadi Sh.milioni 3.5 katika maandalizi ya bajeti ya 2022/23 waliishauri serikali ikapunguza hadi Sh.milioni 2.79 na kuomba kwa mwaka ujao ipunguzwe tena ili waweze kuilipa.

"Kutokana na serikali sasa inahitaji mapato na inataka kukusanya Sh.bilioni 141 tumeona tuje tuwaambie kodi ni kubwa lakini tuwape vyanzo vingine vya kodi ili kufikia malengo yao ambayo katika malori yaliyo chini yetu 26,000, serikali itakusanya zaidi ya Sh.Bilioni 227 bila kuwasumbua wasafirishaji,"alisema.

Alibainisha kuwa kodi inayotozwa kwa sasa kwa mmiliki anayeanzisha biashara imesababisha baadhi ya kampuni zikimbilie kusajili nchi jirani zenye unafuu na ambazo hazina kodi hiyo. Alisema gharama za uendeshaji ni kubwa ni vyema serikali ikawasikiliza wadau hao, kwamba watu wasikimbie kwenda Zambia kusajili halafu kurudi kufanya kazi Tanzania.

"Kama serikali isipopunguza wengi tutapotea kwenye ramani ya biashara na tutashindwa kukua, kitakachofuata msongamano utarudi tena bandarini maana wasafirishaji watapungua na wateja watakimbilia bandari zingine, tunaomba sana serikali iliangalie hili sisi sote ni Watanzania na hatujakataa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yetu,"alisema.

Shabani alishauri serikali ijiepushe na kodi ya makadirio inayofanywa na wafanyakazi wa TRA kwa kuwa wengine siyo waaminifu kutokana na Watanzania wengi kutokuwa na elimu ya kodi.



Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda (kushoto), akizungumza jijini Dodoma juzi, wakati akifungua kikao cha viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, kwa ajili ya maandalizi ya siku ya maridhiano inayotarajiwa kufanyika Machi 3 mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mfumo stakabadhi ghalani wakusanya kilo bilioni 2 za mazao

**Na Paul Mabeja,**DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) Asangye Bangu, amesema tangu kuanza kutumika kwa mfumo huo, umetekelezwa katika mazao 11 na kukusanywa zaidi ya kilo bilioni 2.3 hadi kufikia robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

Bangu alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za bodi hiyo kwa waandishi wa habari.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi za ghala mwaka 2007, zaidi ya kilo bilioni 2.3 za mazao mbalimbali zimekusanywa katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tangu kuanza kwa mfumo huu tumefanikiwa kukusanya zaidi ya kilo bilioni 2.3 za mazao 11 yaliyomo kwenye mfumo mazao hayo ni alizeti, choroko, dengu, kahawa, kakao, korosho, mahindi mbaazi, mpunga, soya pamoja na ufuta,"alisema.

Alisema mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi za ghala ni pamoja na ongezeko la bei za mazao, mapato ya mkulima na mapato ya serikali kwa wastani wa asilimia 200 kutokana na urasimishaji.

"Mafanikio mengine ni ongezeko la uzalishaji wa mazao kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka, mfumo huu pia ni kichocheo cha ubora wa mazao yanayofikishwa sokoni, upatikanaji wa takwimu sahihi za mazao yanayopita kwenye mfumo wa stakabadhi za ghala, ongezeko la mapato ya uhakika kwa serikali kuu na serikali za mitaa, kukuza huduma za fedha vijijini, kufanikisha uanzishaji wa soko la bidhaa Tanzania"alisisitiza

Aidha, alisema tangu kuanzishwa kwa mfumo huo 2007/08 hadi 2020/21 uzalishaji umeongezeka kwa wastani wa asilimia 12 kwa mwaka ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia mbili kwa mwaka kabla ya kuanzishwa.

Pia, alisema katika kipindi cha miezi sita iliyopita bodi imekuwa ikishirikiana kwa karibu na kuhamasisha Bodi ya TEHAMA kukamilisha mifumo mipya na kuhamishia huduma zake kwenda kidijitali.

Alisema bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo, Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) imeanza maandalizi ya kuingiza bidhaa za mifugo ikiwemo ngozi ghafi, ngozi iliyochakatwa na wanyama hai wakiwepo ng'ombe, mbuzi na kondoo.



# ‘Wakurugenzi, mameneja vumbueni vyanzo vya maji’

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKURUGENZI wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira nchini na mameneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wametakiwa kubuni vyanzo endelevu vya maji ili miradi wanayotekeleza kwenye maeneo yao iwahudumie wananchi na kudumu kwa muda mrefu.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi alitoa agizo hilo juzi wilayani Chunya mkoani Mbeya alipotembelea chanzo cha maji cha Mto Gwaziva.

Mahundi alisema Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa maeneo nchini ambayo yananufaika na mradi wa miji 28 ambayo inatakiwa kunufaika kwa kusambaziwa maji kupitia mkopo wa Benki ya Exim ya nchini India.

Alisema kwenye upembuzi wa awali mkandarasi aliyepewa zabuni ya kutekeleza mradi huo wilayani Chunya alitaka kuchimba visima lakini wataalamu walishauri kwamba maji yanayotokana na chanzo hicho hayafai kwa Wilaya ya Chunya kutokana na kuwa na magadi mengi.

Alisema vilevile walibaini kwamba maji ya visima kwa Wilaya ya Chunya siyo endelevu kutokana na hali ya hewa ya eneo hilo hali ambayo ingekuwa inasababisha maji hayo kukauka kwa baadhi ya misimu.

Mkurugenzi wa Ufundi wa RUWASA kutoka makao makuu, Mhandisi Ndele Mengo alisema chanzo hicho hakina gharama kubwa kutokana na kwamba kitasafirisha maji kwa njia ya mserereko na hivyo hakitahitaji nishati ya umeme.

Vilevile alisema chanzo cha aina hiyo ni kizuri kwa sababu gharama ya kutibu maji inakuwa ndogo kuliko wangetumia visima ambavyo kwa wilaya hiyo maji yana magadi mengi.

Alisema chanzo hicho ni cha uhakika na kitasaidia kutatua tatizo la uhaba wa maji kwa wananchi wa Wilaya ya Chunya ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikikabiliwa na tatizo hilo.

Vilevile alisema chanzo hicho kitasaidia kuondoa tatizo la wananchi kukumbwa na tatizo la magonjwa ya mlipuko kikiwemo kipindupindu na magonjwa ya matumbo ambayo yamekuwa yakisababishwa na matumizi ya maji yasiyokuwa safi na salama.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Wilaya ya Chunya, Francis Mwampashi alisema mahitaji ya maji katika Wilaya ya Chunya ni Lita za ujazo 2,500 kwa siku lakini uwezo wa uzalishaji ni lita za ujazo 1,080 kwa siku na hivyo kuwa na upungufu wa zaidi ya asilimia 57.

Alisema walipochunguza chanzo hicho cha Mto Gwaziva walibaini kuwa kina uwezo wa kuzalisha lita za ujazo 7,000 na hivyo kumaliza kabisa tatizo la maji na kuwa na ziada ya lita za ujazo 4,500.

Alisema chanzo hicho ni endelevu kwa sababu maji hayapungui hata ikiwa ni kipindi cha kiangazi kikali na hivyo akasisitiza kuwa ni chanzo cha uhakika.



Mkurugenzi wa Ufundi wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Ndele Mengo (kushoto), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (katikati) juzi, kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Gwaziva unaopeleka maji Chunya mkoani Mbeya. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Chunya, Francis Mwampashi. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

## Mbunge aiangukia serikali ujenzi wa barabara za mikoa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza ameiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa barabara zinazounganisha Mkoa wa Mbeya na Songwe ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji katika maeneo hayo.

Alitoa ombi hilo kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa barabara ya njia nne kutoka katika eneo la Nsalaga jijini Mbeya mpaka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Alisema zipo barabara kuu mbili ambazo ni muhimu lakini kwa muda mrefu wananchi wamekuwa wakiahidiwa kuwa zitajengwa kwa kiwango cha lami lakini utekelezaji haufanyiki.

Alizitaja barabara hizo kuwa ni Mbalizi-Shigamba-Isongole zenye urefu wa zaidi ya Km. 59 ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Songwe kupitia Wilaya ya Ileje na Barabara ya Mbalizi-Mkwajuni-Makongolosi ambayo inaunganisha mikoa hiyo kupitia Wilaya ya Songwe.

“Barabara hizi ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa maeneo haya, zinatumika kusafirisha wananchi na bidhaa mbalimbali yakiwamo mazao mbalimbali wanayozalisha.

Alisema barabara hizo zikijengwa kwa kiwango cha lami zitasaidia kuvutia wawekezaji kutoka katika maeneo mbalimbali ambao watawekeza kwenye sekta za kilimo, uvuvi na uchimbaji wa madini.

Akijibu ombi hilo, Waziri Mbarawa alisema barabara hizo zipo kwenye mipango ya serikali ya kuziboresha ili kuondoa kero ambazo zimekuwa zikiwakabili wananchi kutokana na ubovu wa miundombinu iliyopo kwa sasa. Alisema lengo la serikali ni kuunganisha mikoa yote nchini kwa barabara za lami na kwamba mbali na barabara hizo lakini pia zipo barabara zingine katika Mkoa wa Mbeya ambazo serikali inakusudia kuzijenga.

Alizitaja baadhi ya barabara hizo kuwa ni pamoja na Katumba-Mbambo Tukuyu, barabara ya Makongolosi-Rungwa ambayo inaunganisha Mkoa wa Mbeya na mikoa ya Tabora na Singida.

# Wakulima waulalamikia mfumo wa usambazaji mbolea

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MFUMO wa usambazaji mbolea ya ruzuku unaotumika kwa sasa umelalamikiwa kuwa unasababisha mawakala kushindwa kuwafikia wakulima vijijini, hali ambayo inawalazimu wakulima kutumia gharama kubwa kuipata.

Malalamiko hayo yalitolewa juzi na wadau wa kilimo wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya wakati wakipewa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu yaliyotolewa na Taasisi ya Bens.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara na Wasambazaji wa Mbolea wilayani Mbarali, Winfrida Merere alisema mfumo huo wa ruzuku umekuwa ukiwatesa wakulima ambao wanalazimika kuifuata bidhaa hiyo umbali mrefu.

Alisema serikali imekuwa ikichelewa kuzilipa kampuni fedha zao hali ambayo inafanya kampuni hizo kusitisha kuwapelekea wasambazaji mbolea kwa kuepuka gharama.

“Kampuni zisipolipwa fedha zinashindwa kutuletea sisi mbolea kwahiyo wakulima hawawezi kuipata kwa wakati na wakulima wetu ni wadogo unakuta anahitaji mfuko mmoja ama miwili ambayo hawezi kuifuata Mbeya,” alisema Winfrida.

Athuman Mgandilwa alisema mfumo huo wa ruzuku una siri ambayo serikali haijaiweka wazi na hivyo akaomba uboreshwe ili wakulima wasipate shida kama wanayopata sasa hivi.

Alisema baadhi ya mbolea ambazo ni muhimu huwa zinaadimika katika kipindi ambacho wakulima wanazihitaji zaidi na hivyo kusababisha mazao yao kuharibika tofauti na matarajio yao.

Baadhi ya wakulima walisema pamoja na kwamba mbolea hizo za ruzuku zinauzwa bei ndogo lakini usumbufu wanaoupata unawafanya wasiione nafuu hiyo ya bei.

Mmoja wa wakulima hao, Venancia Katuli alisema mbolea hizo za ruzuku zinapatikana maeneo ya mjini pekee lakini kwenye maeneo yao ambako ndiko kwenye mashamba haipo.

Alisema wanalazimika kuifuata maeneo ya mjini kwa kutumia gharama kubwa jambo ambalo linawafanya wasiione nafuu hiyo inayoelezwa na serikali.

Ofisa Mauzo wa Kampuni ya Bens Agrostar ltd yenye dhamana ya kusambaza mbolea ya fomi inayotengenezwa na kiwanda cha ndani kilichopo mkoani Dodoma, Sunday Adikimu alisema wameanza kuchukua hatua ya kuondoa matatizo hayo.

Alisema wameanza kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea hizo kabla ya kuanza kuitisha vikao vya wadau mbalimbali ili kujadiliana namna ya kuyaondoa matatizo hayo.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Erasto Mwanisao alisema serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha mfumo wa upatikanaji wa mbolea na kwamba hatua ya ruzuku ni mojawapo.






Kaimu Meneja wa Elimu ya Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Makame Khamis akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mazizini Zanzibar jana, kuhusu tuhuma za ukwepaji wa kodi unaofanywa na kampuni ya MGW 2014 Enterprises inayotuhumiwa kujihusisha na uingizaji wa vileo kwa njia za magendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ZAECA kuwahoji maofisa ZLB kuhusu uingizaji vileo

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) imesema itawaita viongozi wa bodi ya vileo Zanzibar (ZLB) kueleza wanasimamia vipi vileo vinavyoingizwa kwa msamaha wa kodi ili kuhakikisha vinatumika kama ilivyokusudiwa.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hiyo, Ali Abdallah Ali, wakati akizungumzia tuhuma za kuhusishwa na magendo ya vileo kwa Kampuni ya MGW 2014 interpreses kupitia taasisi moja ya ulinzi na usalama visiwani Zanzibar.

Alisema kwamba suala la kudhibiti magendo na mianya ya ukwepaji kodi kuna taasisi husika zinasimamia majukumu hayo, lakini ZAECA italazimika kuwaita viongozi wa bodi ili kufahamu wanasimamia vipi bidhaa zinazoingizwa Zanzibar kwa misamaha ya kodi bila ya kuathiri ukusanyaji wa mapato na kuibuka magendo.

"Kama ZAECA watu wetu wanafuatilia tuhuma hizo lakini tutawaandikia barua ya wito viongozi wa bodi ya vileo watuambie wanasimamia vipi bidhaa zinazoingizwa Zanzibar na kunufaika na msamaha wa kodi ili kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa," alisema. Kaimu Meneja wa Elimu ya Mlipa kodi wa Mamlaka ya ZRA, Makame Khamis alisema kampuni tatu ndizo zilizopewa vibali vya kuingiza vileo kutoka nje ya Zanzibar tangu kuanza kutumika Sheria ya Vileo ya Mwaka 2020.

"Kampuni zinazoruhusiwa kuingiza vileo Zanzibar ni One Stop Center, SCOCH na ZMMI na kampuni zingine za vileo zilizosajiliwa Zanzibar zinapaswa kununua vileo kutoka kampuni hizo na kusambaza kwa wateja wao",alisema Makame.

Kuhusu sakata la Kampuni ya MGW 2014 Interprises, alisema wanafanya uchunguzi na endapo watabaini hatua za kisheria zitachukuliwa.

Alisema tatizo la magendo litadhibitiwa Zanzibar iwapo wananchi watashirikiana na vyombo vyenye dhamana vya kusimamia kodi na uzidhibiti wa magendo kuhakikisha wanatoa taarifa za siri kabla ya biashara ya magendo kufanyika.

"Wito wangu kwa wananchi kuwa tayari kusaidia kutoa taarifa za siri kwa watu wanaojihusisha na biashara za magendo kwa vile kodi ndiyo msingi wa maendeleo ya Zanzibar"alisema Makame.

Naibu Kamishna wa Mamlaka ya kodi ya mapato Tanzania (TRA) Juma Bakari Hassan, alisema kwamba shehena ya vileo iliyoingizwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania JWTZ iliruhusiwa kutoka katika Bandari ya Malindi Zanzibar baada ya kukamilisha kulipa tozo ya miundombinu ya Shilingi milioni 15.7 kabla ya kuruhusiwa kuteremshwa bandarini hapo.

Alisema kodi ndiyo chanzo cha mapato ya serikali katika maendeleo ya nchi na kuwataka wananchi kujenga utamaduni wa kutoa taarifa za siri dhidi ya kampuni zinazojihusisha na biashara za magendo na kusababisha mianya ya ukwepaji wa kodi.

Akizungumzia kuhusu kampuni yake kuhusishwa na biashara ya magendo ya vileo kupitia taasisi moja ya ulinzi na usalama, msimamizi wa Kampuni ya GMW 2014 Interpreses, Ali Seif alikanusha kampuni yake haihusiki na biashara ya magendo ya vileo.

# Wizara ya Kilimo yaanza kukabiliana na tatizo la sumukuvu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo imesema kuwa katika kukabiliana na tatizo la sumukuvu wamefanya utafiti ili kujua hali halisi ya tatizo nchini.

Imesema matokeo yameonesha uwapo wa tatizo kwenye mazao ya mahindi, njugu nyasa na pilipili manga.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameri Abdallah.

Waziri huyo alisema pia wizara imeandaa rasimu za kanuni mbili za kudhibiti wa sumukuvu.

"Kanuni hizi zimetayarishwa chini ya Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe inayosimamiwa na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na Sheria ya Chakula na Dawa inayosimamiwa na Wakala wa Chakula na Madawa, Zanzibar (ZFDA),"alisema.

Alisema wizara inakamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhi nafaka ili kupunguza uwepo wa tatizo la sumukuvu kwa vile moja ya sababu ya kuenea kwake ni uhifadhi mbaya wa mazao ya nafaka.

Waziri huyo alisema wizara yake imefanya mafunzo kwa wakulima 1,853 juu ya njia bora za kilimo na utunzaji bora wa mazao baada ya kuvuna.

# Dk. Mwinyi aomba Puma Energy kupunguza bei ya mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imeitaka Kampuni ya Puma Energy kuangalia uwezekano wa kupunguza bei ya mafuta ya ndege ili kuendana na soko la ushindani la kimataifa.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi alisema hayo wakati akizungumza na uongozi wa kampuni hiyo, Ikulu Zanzibar, alisema ongezeko la bei ya mafuta kwa kampuni hiyo inaiathiri Zanzibar kwa baadhi ya kampuni kubwa za ndege kushindwa kutua nchini kwa hofu ya kukosa mafuta.

Hivyo, aliishauri kampuni hiyo kushusha bei ili kuendana na soko la ushindani hasa kwa kampuni za usafiri wa anga na wadau wingine kwenye sekta ya usafirishaji.

Alisema kuna mgogoro mkubwa kwenye sekta hizo uliosababishwa na kupandisha gharama za mafuta ya ndege, hali inayosababisha baadhi ya kampuni kubwa za ndege kununua Dar es Salaam na Mombasa.

Aidha, Dk. Mwinyi alieleza wanaoathirika zaidi ni kampuni ndogo za ndege zinazofanya safari zake za ndani baina ya Pemba, Tanga na Dar es Salaam.

Hata hivyo, aliwashauri Puma Energy kutoridhika na hali hiyo, badala yake wakubaliane na hali halisi ya soko la ushindani lilivyo ili kutoa fursa ya soko la biashara kwa kila mwekezaji.

Aliwaeleza kampuni hiyo endapo watashindwa punguguza gharama za mafuta na kukabiliana na ushindani wa kibiashara uliopo kwenye usafirishaji wa anga, Serikali tayari imeiagiza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kuangalia uwezekano wa kampuni nyingine kupewa fursa ya kuhudumia eneo hilo.

Alisema Serikali ina dhamira njema kwa wawekezaji wote pia inaunga mkono jitihada wanazozifanya kwa Serikali katika kuwahudumia watu na mazingira mazuri ya biashara, hivyo aliwataka wawekezaji kukabiliana na ushindani kwa kuleta unafuu kwa kila mmoja.

Pia Dk. Mwinyi alieleza Serikali imedhamiria kufanya uwekezaji mkubwa wa kuhifadhi mafuta ya kutosha ili kujiweka tayari na tatizo lololote.

Aliishauri Kampuni ya Puma Energy kuangalia fursa za uwekezaji wa eneo hilo kwa Bandari ya Mangapwaji kuweka chemba ya kushushia mafuta na ghala la kuhifadhia mafuta ya ndege.

Alisema Serikali inajipanga kuhifadhi mafuta ya ziada ili iwe na uwezo wa kukabiliana na changamoto itakayotokea kwa kuziba mianya ya athari za changamoto hizo.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Kanda ya Afrika, Fadi Mitri alisema kwamba wana nia njema ya kuwekeza Pemba kwenye uwanja mpya wa ndege wa kimataifa kuwa wa kisasa na bora zaidi kwa Afrika nzima kuongoza kwa huduma za kimataifa na vifaa vyenye ubora wa uhakika.

Alisema Kampuni ya Puma Energy itawekeza kwenye miundombinu ya kisasa ya uwanja huo, ipo tayari kutoa huduma za ndege za kimataifa kwenye uwanja huo.

Aidha, aliiahidi Serikali kuongeza ndege zaidi za kimataifa kuja moja kwa moja Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DAVID MADUHU MAIGE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili

**T 916 DPJ - TOYOTA RACTIS.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi:**

**DSM/PHQ/RB/63788/2023.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT COURT OF MBEYA**
**AT MBEYA**
**PROBATE CAUSE NO 01 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF**
**THE LATE GREGORY MWAKAJE ISOTE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR PROBATE CAUSE BY**
**GEOFREY GREGORY ISOTE**
**PETTTIONER**
**PETITION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**GENERAL CITATION**

**[Rule 75 of probate Rule made under section 9of the probate and administration of Estates Act Cap 352 R.E 2002]**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are here by cited to come and see the proceedings before the grand of probate [or letter of Administration] is made to the named petitioner.

Objection to the grant should be filled before or on 14 day of March, 2023

**Dated at Mbeya this 14 day of February 2023.**

A. P. SCOUT
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE COURT
MBEYA

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **PHILBERT BINAMUNGU BENEDICTO** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari lenye namba za usajili **T 798 AYT**, injini namba **IHZ0193917** na chassis namba **HZJ750033856.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/62776/2023.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0785557979.**

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NO. 91/2022**
**DEOGRATIAS ELENEUS MTITU..................MDAI**
**DHIDI YA**

- **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC.............MDAIWA**
- **BARAKA PAUL DABAVUNJE................MDAIWA**
- **JOHALI YUDA MAHENGE..............MDAIWA**
- **ZAINABU JUNUSI.................MDAIWA**
- **GIBSON EDWARD....................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: BARAKA PAUL DABAVUNJE, ZAINABU JUNUSI NA GIBSON EDWARD**

**Fahamu kwamba DEOGRATIAS ELENEUS MTITU amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili.**

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/02/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. A. Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya. Mnaarifiwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.

Kumbuka: Usipo hudhuria siku hiyo Baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

**Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo tarehe 30/01/2023.**

A. Mapunda
MWENYEKITI
30/01/2023

---

## KUPOTELEWA NA KADI ZA BAJAJI

**JOHN MUSSA KOMBO**

anatangaza kupotelewa na kadi za Bajaji zenje namba za usajili

**MC CNH998** na **MC CNH996**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa za polisi:

**DSM/PHQ/RB/57407/2023** na **DSM/PHQ/RB/57409/2023.**

---

## KUPOTELEWA NA CHETI



**NOELA ROGARTH MINDE** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba chenye index number **PS0703027-031** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. ANNE PRIMARY SCHOOL** mwaka **2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/65602/2023.**

---

**FORM 5B**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 130 OF 2023**
**In the Matter of the Late ZAWADI SALUM KHALFAN**
**and**
**In the Matter of Application for latters of administration**
**by**
**BARAKA SALUM KHALFAN**

**GENERAL CITIATION**
**(Rule 75)**

**All Persons** claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the preceedings if they think fit before the grant of probate (or latters of administration) is made to the above -named patitioner.

Objections of the grant should be filed on or before the **24** day of **04, 2023.**

Dated at **DAR ES SALAAM** this **13** day of **02, 2023**

Senior Resident Magistrate

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**BERTHA MTUYA KABALIKA**

anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja Namba **756** kitalu **'M'** chenye jina la **JAMES MWAKABUNGU** kilichopo Forest Mbeya. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi:

**IRI/IRI/RB/59961/2023.**

---

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda**
**Wilaya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 11/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**RIGHTON OSINGI GWAKISA WA AREA FIVE**
**KATIKA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LUSAJO GWAKISA KAMWELA**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24/ Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 15 mwezi 02 mwaka 2023**

---

## KUPOTELEWA NA KADI HALISI ZA PIKIPIKI

**KAMPUNI YA GOLDSTAR PAINTS** TANZANIA LIMITED, INAYO JIHUSISHA NA UTENGENEZAJI RANGI TANZANIA BARA. INATANGAZA KUPOTELEWA NA "KADI HALISI ZA PIKIPIKI; NAMBA **MC 307 CLW, MC 368 BLQ NA MC 457 CPP** ZIMESAJILIWA KWA JINA LA GOLDSTAR PAINTS TANZANIA LIMITED, ZIME TOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA).

***DSM/PHQ/RB/49666/2023**

HIVYO KWA YEYOTE ATAKAE ZIOKOTA ANAOMBWA KUZIWASILISHA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI / OFISI ZA GOLDSTAR PAINTS TANZANIA LIMITED AU AWASILIANE NASI KUPITIA NO **+255 759 003 979/+255 752 022 066.** AHSANTENI.

---

## NAFASI ZA KAZI

**KIWANDA KIPYA CHA KUSAGA NAFAKA [MILLING] KILICHOPO MLANDIZI, KIBAHA KINAAJILI NAFASI ZIFUATAZO**

1. Chief Miller (1)
2. Industrial Electrical & Mechanical engineer (1)/technician (2)
3. Motor vehicles technicians (2)
4. Food Quality Control Manager (1)/ Food Quality Control Officer (2)
5. Accounts & Finance Manager (1) /Accounts & Finance Officer (2)
6. Admin and Customer Service Officer (2)

Tuma CV, transcripts na barua ya maombi kwa email hii **hr.grainsmill.uk@gmail.com**

*Closing date: Two weeks from the date of advertisement appeared in the Newspaper. Please note that only shortlisted candidates will be contacted.*






**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## China, Iran zataka vikwazo kuondolewa

**BEIJING,** CHINA

RAIS wa China Xi Jinping na Ebrahim Raisi wa Iran, wametoa mwito wa kuondolewa kwa vikwazo nchini Iran, kama sehemu muhimu ya makubaliano ya kimataifa yaliyokwama kuhusiana na mpango wa nyuklia wa nchi hiyo.

Viongozi hao walisema vikwazo vyote vinatakiwa kuondolewa kwa namna inayofaa ili kuhamasisha utekelezwaji kamili wa makubaliano hayo ya kimataifa ya mwaka 2015.

Raisi kwa upande wake alisisitiza kwamba Iran haitakubaliana na hatua zinazoegemea upande mmoja, china-yaiahidi-iran-uungwaji-mkono-thabiti/a-64699968" ukandamizaji na vikwazo, ambavyo kwa pamoja vinadhoofisha amani na maendeleo na kuvuruga mfumo wa ulimwengu.

Wakuu hao wawili walitoa mwito huo katika taarifa yao ya pamoja, ikiwa ni siku ya mwisho ya ziara ya Raisi nchini China.

Aidha, china-yataka-kutatua-utata-mkataba-wa-nyuklia-wa-iran/a-64700498" Xi amekubali mwaliko kutoka kwa Raisi wa kuzuru Iran na kuahidi kufanya hivyo katika wakati muafaka.**DW**

## Armenia yaweka mpango wa amani

**YEREVAN,** ARMENIA

ARMENIA imewasilisha mpango wa makubaliano ya amani kwa hasimu wake Arzebaijan ili kumaliza mvutano uliodumu kwa miongo kadhaa juu ya jimbo la Nargono-Karabakh.

Waziri mkuu wa HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/armenia-yaiomba-icj-kuiamuru-azerbaijan-kuondoa-vizuizi/a-64558989" Armenia, Nikol Pashinyan, ameliambia baraza la mawaziri jana, kuwa walikamilisha sehemu nyingine ya makubaliano hayo ya amani na yanayolenga kuanzisha mahusiano ya kidiplomasia baina yao na Arzebaijan.

Tangazo hili linatolewa baada ya Armenia kuituhumu Arzebaijan kwa kutekeleza sera ya safishasafisha ya kikabila na kuwalazimisha watu wa kabila ya Armenia kuondoka kwenye jimbo hilo lililojitenga.

Mataifa hayo mawili HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/umoja-wa-ulaya-kutuma-ujumbe-wake-armenia/a-63365722" yamepigana vita mara mbili yakizozania udhibiti wa jimbo hilo la Azerbaijan lenye wakazi wengi wa Armenia na kusababisha vifo vingi vya raia. **DW**

# Watano wakutwa hai chini ya kifusi

**ANKARA,** UTURUKI

WANAWAKE watatu na watoto wawili wamepatikana wakiwa hai chini ya kifusi baada ya siku tisa tangu kutokea kwa maafa ya tetemeko la ardhi nchini Uturuki.

Melike Imamoglu (42) na Cemile Kekec (74) walitolewa kwenye vifusi na waokoaji katika mji wa Kahramanmaras nchini humo.

Uokoaji wao ulikuja wakati wafanyakazi walielekeza umakini wao katika kusafisha miji iliyoharibiwa na matetemeko ya ardhi ya hivi karibuni.

Mamilioni ya watu nchini Syria na Uturuki wanaishi katika kambi za muda na wanahitaji msaada wa kibinadamu.

Video ya uokoaji iliyotumwa kwenye mitandao ya kijamii na Meya wa Darica, Muzaffer Biyik, ilionyesha wafanyakazi wakipiga makofi na kukumbatiana huku Kekec akiingizwa kwenye gari la wagonjwa.

Huko Antakya, mji mwingine wa Uturuki ulioathiriwa vibaya na matetemeko ya ardhi, vyombo vya habari vya ndani viliripoti kwamba mama na watoto wake wawili walitolewa wakiwa hai kwenye vifusi.

Siku kumi baada ya tukio hilo, inakuwa vigumu kupata manusura wa tetemeko hilo.

Hata hivyo idadi ya vifo vilivyojumuishwa inafikia zaidi ya 41,000.

Waokoaji wa kigeni waliowasili Uturuki muda mfupi baada ya matetemeko hayo, wanaanza kufungasha virago na kurejea nyumbani, huku wenyeji wakielekeza nguvu zao katika kuondoa vifusi vya majengo yaliyoporomoka na kusafisha miji.

**BBC**



Wafanyakazi wa dharura wa Ukraine na wa kujitolea wakimbeba mwanamke mjamzito aliyejeruhiwa kutoka hospitali ya uzazi iliyoharibiwa na shambulio la anga huko Mariupol, Ukraine.**PICHA:AP**

# Marekani kulitangaza kundi la Wagner kuwa la kigaidi

**WASHINGTON,** MAREKANI

WABUNGE WA SENETI nchini Marekani kutoka vyama vyote viwili vya kisiasa, wametangaza nia yao kuliweka kundi la mamluki la Russia la Wagner, kama shirika la kigeni la kigaidi.

Maseneta wananuia kupitisha muswada huo ambao utalazimisha Idara ya mashauri ya ndani kufanya mabadiliko yanayohitajika.

Wanaounga mkono ushirikiano kwa Ukraine na kuongezeka kwa shinikizo kwa Russia kati ya wabunge wa Marekani katika mwaka uliopita, kumeishinikiza serikali kujumuisha kundi la Wagner kwenye orodha ya mashirika ya kigaidi.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, Idara ya Hazina ya Marekani ilitangaza kampuni inayoongozwa na Yevgeny Prigozhin kuwa shirika kubwa la uhalifu wa kimataifa na iliweka vikwazo kwa makampuni kadhaa na watu binafsi wanaohusishwa nayo.

Hatua hiyo itaifanya Wagner kuwa sawa na makundi ya mafia ya Italia au makundi ya uhalifu wa kupanga kutoka Russia na Japan.

Kulingana na kundi la wabunge wanaoongozwa na Ben Cardin wa Democratic na Roger Wicker wa Republican, hatia hiyo haitoshi kuwaadhibu.

Maseneta walitangaza kuanzishwa upya kwa muswada katika kuwawajibisha mamluki wa Russia.

Iwapo itatambuliwa kama shirika la kigaidi, itakuwa ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote nchini Marekani kuipatia msaada wa aina yoyote.

Hatua hiyo itagusa pamoja na miamala ya kifedha, mafunzo, kutoa silaha au huduma za ushauri.

Katika baadhi ya matukio, inaweza pia kusababisha kufukuzwa kwa wanachama wa shirika hilo nje ya Marekani.

Wakati huo huo, limegundulika eneo jipya la mazishi la watu ambao huenda walipigana katika eneo la Ukraine kama sehemu ya kundi la Wagner.

Kulingana na PMC, ndugu na jamaa za baadhi ya waathiriwa hawakujua kuhusu vifo vyao na waliambia BBC kuwa wamekuwa wakijaribu kujua hatima yao kwa miezi kadhaa.

Mwanzoni mwa Februari, wakazi wa Luhansk waligundua makaburi mapya 42 ya wanaume kwenye eneo la jirani na hapo.

Wakazi wa kijiji cha Kirovka, kilicho karibu na makaburi hayo, walisema kwamba hakuna mtu anayetembelea makaburi hayo, na hakuna hata mmoja wa waliozikwa anayejulikana .

"Tulifikiri ghafla hawa watu wamelala hapa na hata ndugu zao hawafahamu, wakapiga picha za makaburi yote, wakaanza kuwagawia kwenye vikundi vya watu waliopotea, na sasa watu tisa wamenijibu. Wote hawakujua hata kwamba wapendwa wao walikufa,"

mmoja wa wanawake aliambia BBC.

BBC iliweza kupata maelezo ya wanaume 37 katika vyanzo vya wazi, ambao data zao zinalingana na maandishi kwenye vibango vya makaburi karibu na Lugansk.

Hata hivyo,35 kati yao walikuwa Warussia, mmoja alikuwa raia wa Belarusi, mwingine alizaliwa Uzbekistan.

Tovuti za mahakama za Russia zilichapisha hukumu za mahakama dhidi ya watu 20 ambao ni majina kamili ya waliozikwa Lugansk. **BBC**

# MASHABIKI SIMBA, YANGA WABANANA BETIKA MTOKO

**Mwandishi Wetu**

MASHABIKI wa soka wa timu kongwe nchini, Simba na Yanga wameanza kutambiana kuelekea mchezo wa watani utakaochezwa Aprili 16, mwaka huu baada ya kila upande kupata mshindi kwenye droo ya kwanza ya Betika Mtoko wa Kibingwa.

Bahame Balele wa Simiyu na Constantine Mbele kutoka Ruvuma wamefungua dimba la kuwa wa kwanza kuingia katika promosheni ya Mtoko wa Kibingwa inayoendeshwa na Kampuni ya Betika nchini.

Februari 7, mwaka huu kampuni hiyo ya kubashiri matokeo ilizindua promosheni ya tano ya Mtoko wa Kibingwa ambayo msimu huu itawagharamia mashabiki 100 kutoka maeneo mbalimbali nchini ili kuishuhudia dabi hiyo yenye upinzani wa jadi.

Kampeni hiyo ya miezi miwili inawapa fursa mashabiki wa soka nchini kujishindia zawadi mbalimbali, kubwa kuliko ikiwa ni kufika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia mtanange huo.

Washindi wa droo ya kwanza kwa nyakati tofauti wamesema hiyo ni mara yao ya kwanza kupata fursa ya kuishuhudia dabi laivu kwani wamekuwa wakiitizama miaka yote kwenye luninga.

"Sijawahi kufika Dar es Salaam, na sikuwa na ndoto hizo, ipo siku nitakwenda kwa ajili ya kuishuhudia dabi, Betika walipozindua kampeni ya Mtoko wa Kibingwa, nilijaribu bahati yangu, sikuwa na matarajio ya kushinda kwani sijawahi kushinda, nashukuru msimu huu nimepata fursa hiyo,"alisema Balele na kuongeza.

"Natamani siku yenyewe ifike, nikaishuhudie Yanga ikikoleza kasi ya ubingwa kwa kumchinja mnyama, sina shaka na timu yangu katika dabi hiyo, naamini tutashinda," alisema shabiki huyo wa Yanga.

Constantine ambaye ni mnazi wa Simba yeye anaamini Aprili 16, mwaka huu watafuta 'uteja' kwa watani zao huku Moses Phiri ndiye mtu anayemtarajia apindue meza ya dabi hiyo.

"Haiwezekani Simba tufungwe na Yanga mfululizo mara tatu, hilo jambo haliwezi kutokea, nawashukuru Betika kwa kutoa fursa kwa mashabiki, ninachokisubiri ni siku tu ifike nikamshuhudie Mnyama akiunguruma kwa Mkapa," alisema.

Meneja Mkuu wa Betika Tanzania, Tumaini Maligana, alisema washindi hao ni wa droo ya kwanza wa wiki iliyopita huku wale wa wiki hii wakitarajiwa kutangazwa wakati wowote kuanzia sasa.

"Tamati ya droo hii itakuwa ni wiki ya mwisho ya siku ya dabi ambapo tutakuwa na washindi 100 wa Mtoko wa Kibingwa," alisema Maligana.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema droo ya Mtoko wa Kibingwa inahusisha pia wachezaji wa Kitonga Jackpoti na Casino Jackpoti ambao wataingia moja kwa moja bila kujali matokeo ya bashiri zao kwenye mikeka hiyo.



Shabiki wa Simba, Bahame Balele (kushoto) na Constantine Mbele wa Yanga kutoka Ruvuma wakiwa katika mahojiano maalumu kuelekea mechi ya watani wa jadi itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu. Mashabiki hao wataletwa Dar es Salaam kushuhudia mechi hiyo kwa gharama ya Kampuni ya Betika Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Doumbia ahitaji muda Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga amesema beki wao wa kati, Mamadou Doumbia, aliyesajiliwa katika dirisha dogo kutoka Mali, anahitaji muda wa kuelewana na wachezaji wenzake.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya beki huyo aliyesajiliwa kutoka klabu ya Stade Malien ya Mali kutoonekana kucheza, hasa katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Monastir na kuongeza hiyo inatokana na kutozoena vyema na mabeki wenzake.

Kamwe alisema pamoja na kiwango chake kizuri alichokuwa nacho, lakini anahitaji muda wa kuzoea vyema mazingira ya kiuchezaji na wenzake na umuhimu wa nafasi anayocheza.

"Kwa sababu anacheza namba tano ambayo ni nafasi nyeti sana kwenye kikosi, yeye na Dickson Job, Yannick Bangala, Bakari Mwamnyeto, anatakiwa kupata muda mwingi wa kucheza kwanza kwenye viwanja vya mazoezi," Kamwe alisema.

Hata hivyo Kamwe aliongeza anaamini wengi wanaomuulizia sana ni kwa sababu walifungwa mabao ya juu dhidi ya Monastir lakini akabainisha siku zote mpira hauchezwi juu tu.

"Wengi wanamuulizia kwa sababu tulifungwa mipira ya juu Jumapili iliyopita, lakini siku zote dakika 90, mpira haichezwi juu tu, ule siyo mpira wa kikapu kuna wakati unawekwa chini na sisi tumeonyesha na kumiliki sana soka la chini, yaliyotokea ni matokeo ya mpira tu. Tayari mwalimu amesema ameanza kuona matokeo chanya kwake, ameshaanza kuzoea mazingira na wenzake pia, hivyo muda si mrefu wanachama na mashabiki wa soka watamwona uwanjani," alisema Kamwe.

# Singida yaikalia kooni Azam FC

**Na Hadija Mngwai**

SINGIDA Big Stars imetamba imejiimarisha tayari kusaka matokeo mazuri kwa lengo la kumaliza Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kwa sasa Singida Big Stars ipo katika nafasi ya tatu baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Ihefu ikiwa imepishana pointi moja na Azam FC yenye alama 43.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Massanza, alisema wamefurahishwa kuona wameishusha Azam FC na sasa wanaendelea kujipanga kuhakikisha wanabakia katika nafasi hiyo hadi mwisho wa msimu.

**Massanza alisema anafahamu ushindani uliopo katika mechi za ligi, lakini wachezaji wao wameahidi kujituma katika kila mechi watakayocheza.**

"Tumefanikiwa kupata alama moja baada ya sare na Ihefu imetusaidia kuvuka daraja na kupanda nafasi ya tatu, kazi nzuri hii ni kutokana na matokeo mazuri na pointi moja tuliyoipata ingetusaidia kufika nafasi ya tatu na kuishusha Azam. Tunaendelea kupambana kuhakikisha tunashinda mechi zetu zote zilizobakia ili kumaliza ligi katika nafasi ya tatu ya msimamo, timu ina ari kubwa katika michezo iliyobakia.

"Tumerejea nyumbani kutoka Mbeya tumewapa mapumziko wachezaji kwa ajili ya kukaa sawa, ukiangalia mchezo unaofuata dhidi ya Mtibwa Sugar upo mbali (Februari 27, mwaka huu), hivyo tumeona tuwape mapumziko mafupi hadi Ijumaa, tutaanza maandalizi kuelekea mchezo huo Jumamosi (kesho)," alisema Massanza.

Wakati huo huo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Kalimangonga Ongala, amesema mechi mbili za kirafiki walizocheza zimempa mwanga na kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kumaliza msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa heshima.

Kalimangonga alisema wanatarajia kupata matokeo chanya kuanzia mechi ijayo dhidi ya Simba na nyingine zilizobakia katika ligi hiyo ya juu nchini.

Azam FC itakuwa na Simba katika mchezo wa raundi ya 24 ya Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Februari 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR ATAKIWA CHELSEA

MMLIKI wa Chelsea, Todd Boehly amekutana na Rais wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi jijini Paris kujadili uwezekano wa uhamisho wa mshambuliaji wa Brazil, Neymar, mwenye umri wa miaka 31, msimu wa joto. (***Le Parisien***)

### ARSENAL YAMTAKA RASHFORD



ARSENAL inafuatilia hali ya mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 25, huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mkataba wake pale Old Trafford. (***Football Insider***)

### ARTETA AMTAJA ZUBIMENDI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta ameitaka klabu hiyo kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Hispania, Martin Zubimendi, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Real Sociedad. (***Sport***)

### DE JONG ALIIKATAA UNITED

KOCHA wa Barcelona, Xavi amesema kiungo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, hakutaka kujiunga na Manchester United msimu uliopita wa joto. (***Sun***)

### ARAUJO KUTUA BARCA

BARCELONA imefikia makubaliano na LA Galaxy kwa ajili ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Mexico, Julian Araujo, mwenye umri wa miaka 21 kwa mkataba utakaoishia ifikapo Juni, mwaka 2026. (***Fabrizio Romano***)

### HINCAPIE ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mlinzi wa Ecuador, Piero Hincapie, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Bayer Leverkusen. (***Caught Offside***)

### VILLA KUMUUZA MARTINEZ

KLABU ya Aston Villa inaweza kusikiliza ofa kwa mlinda mlango wa Argentina, Emiliano Martinez, mwenye umri wa miaka 30, ili kusaidia kufadhili ujenzi wa klabu hiyo msimu wa joto. (***Mirror***)

### CANCELO AKANUSHA UVUMI

MLINZI wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 28 amesema tetesi alitofautiana na Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, kabla ya uhamisho wake wa mkopo kwenda Bayern Munich ni "uongo mtupu". (***Mundo Deportivo, via Mirror***)

### POCHETTINO KUREJEA

KOCHA, Mauricio Pochettino anaweza kurejea kuiongoza Tottenham Hotspur kwa kuchukua nafasi ya Antonio Conte. (***TalkSPORT***)

### PAEZ AGEUKA LULU

CHELSEA, Liverpool, Manchester City, Manchester United na Newcastle United zimewasiliana na klabu ya Independiente del Valle ya Ecuador kuhusu kiungo wa kati, Kendry Paez, mwenye umri wa miaka 15. (***90min***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AELEZA SIRI KUAMBULIA KICHAPO

**Ni ubora wa hali ya juu ulioonyeshwa na City katika mechi hiyo lakini...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisikitishwa na makosa ya Arsenal yaliyoipa Manchester City ushindi na pigo kubwa la kisaikolojia katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England msimu huu.

Manchester City inayonolewa na Kocha, Pep Guardiola, ilipambana na kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Emirates na kuwatangulia Arsenal, ambao wamecheza mechi chache zaidi, kwa tofauti ya mabao kwenye kilele cha Ligi Kuu England.

Kevin De Bruyne aliadhibu pasi mbovu ya Takehiro Tomiyasu na kufungua ukurasa wa mabao kabla ya magoli ya kipindi cha pili kutoka kwa Jack Grealish na Erling Haaland, huku bao la Arsenal likifungwa na Bukayo Saka kwa mkwaju wa penalti.

Arteta, ambaye alikuwa msaidizi wake katika kikosi cha City chini ya Guardiola kabla ya kuchukua jukumu la kuwa Kocha Mkuu wa Arsenal, alikiri washikabunduki hao waliadhibiwa kwa kuonyesha makosa yao Kaskazini mwa London.

"Tulipoteza, ilikuwa vita ya ajabu dhidi ya timu mbili na tulikuwa nazo, lakini tuliwapa mabao," alisema Arteta, ambaye amepoteza michezo minane kati ya tisa dhidi ya Guardiola katika mashindano yote, akiiambia Amazon Prime Video.

"Tulikuwa nao katika nyakati kubwa, lakini katika nyakati kubwa walikuwa bora kuliko sisi. Kwa kweli hatukuwa sahihi, tulijiweka kwenye matatizo, katika baadhi ya maeneo ya uwanja tulicheza kupita kiasi na tukaadhibiwa.

"Tulipata nafasi tatu kubwa, lakini hatukuziweka pembeni na hiyo ndiyo ilikuwa tofauti. Ili kuwafunga ni lazima tuwe juu ya kiwango chetu kwa sababu ni timu nzuri.

"Hali ya anga na utendaji ulikuwa mzuri sana, ukiondoa jinsi tulivyowapa mabao matatu."

Licha ya kushindwa, Arteta amesema uchezaji huo ulisaidia tu kuendeleza imani yake Arsenal wanaweza kutwaa taji lao la kwanza tangu msimu wa 2003-04.

"Nina imani zaidi kuliko nilivyokuwa kabla ya mchezo, na kiwango ambacho timu ilikuwa nayo dhidi ya City," aliongeza.

Baada ya kucheza mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu England bila kushinda, Arsenal watasafiri kucheza na Aston Villa hapo kesho.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,077,4
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13


KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KARIM BENZEMA AMPIKU RAUL UFUNGAJI BORA



**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema amempita Raul na kuwa mfungaji bora wa pili wa Real Madrid wa wakati wote kwenye Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga.

Benzema alifikisha mabao 229 ya LaLiga, katika mechi 428 katika kinyang'anyiro hicho, alipofunga kwa penalti na kuwafanya vijana wa Carlo Ancelotti kuongoza ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Elche hapo juzi.

Bao zuri kabisa la Marcos Asensio liliwapa Los Blancos uongozi wa mapema kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, huku Benzema akizidisha faida yao nusu saa baada ya Enzo Roco kujifunga kwenye eneo la hatari la Elche.

Benzema alifunga bao lake la 230 la LaLiga kabla ya kipindi cha kwanza kwenda mapumziko, akifunga bao lake la pili kwenye mechi hiyo.

Nyota wa zamani wa Madrid, Raul ilimchukua mechi 550 na kufikisha mabao 228 kwenye LaLiga, hiyo ikimaanisha Benzema amempita katika mechi 122.

Cristiano Ronaldo, ambaye ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa Madrid, anasimama mbele ya Benzema kwa mabao 311 katika mechi 292 za LaLiga.

Benzema tayari alikuwa mfungaji bora wa pili kwa Madrid katika mashindano yote, baada ya kumpita Raul mwaka jana.



# Dybala hataki kuondoka Roma

**ROME,** Italia

MSHINDI wa Kombe la Dunia, Paulo Dybala, amesema hajui chochote kuhusu mustakabali wake ndani ya AS Roma.

Mshambuliaji huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 29 aliondoka Juventus kwa uhamisho bure kwenda Roma kwa mkataba wa miaka mitatu mwaka jana, lakini amekuwa akihusishwa na Manchester United.

Dybala amevutia sana akiwa na Giallorossi hao msimu huu, akifunga mabao 11 na kutoa asisti saba katika mechi 21 alizocheza.

Hata hivyo, inasemekana ana kipengele cha kuachiwa kwa pauni milioni 10.7 katika mkataba wake, ambacho kinaweza kuchochewa na klabu za nje ya Serie A, huku Dybala akipinga uvumi huo wa United.

Alisema: "Inapokuja kwa kifungu changu cha kutolewa, kama nilivyosema hapo awali ni kitu kati ya wakala wangu na klabu.

"Siwezi kujua nini kitatokea mwishoni mwa mwaka."

Kocha wa Roma, Jose Mourinho, pia amekuwa mada ya uvumi hivi karibuni, licha ya kuwa chini ya mkataba hadi 2024.

Dybala anatumaini Mourinho atasalia na klabu hiyo na anatamani kushinda kombe chini ya kocha ambaye anamwita 'mmoja wa mameneja bora zaidi duniani'.

-33,324/-



# RUVU SHOOTING HOFU IKIWAVAA GEITA GOLD

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena leo wakati Ruvu Shooting itakapokuwa ugenini kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu kuwakabili Geita Gold FC.

Ni mechi itakayozikutanisha timu mbili zenye malengo tofauti kwenye ligi hiyo, Geita Gold ikiwa inasaka nafasi moja kati zile nne za juu wakati Ruvu Shooting inapigania uhai wake kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire (pichani), alisema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wanazitaka pointi tatu kwa 'udi na uvumba' ingawa wanafahamu ugumu wa kupata ushindi kwenye uwanja wa Nyankumbu.

"Lengo ni kuhakikisha dakika 90 zinaleta matunda tupate pointi tatu. Tunafahamu Geita Gold wako vizuri, moja ya timu ambazo si za kubeza hasa zinapokuwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, lakini umuhimu wa uhitaji wa pointi hizo, tumechukua tahadhari kubwa mno, tumejidhatiti kila eneo, tumefanya masahihisho na maboresho ambapo tuna uhakika kushinda. Ushindi wetu utawaongezea vijana hamasa ya kufanya vyema katika mechi zinazofuata," alisema Masau.

Geita Gold inashika nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 31 na inanyemelea nafasi moja kati ya nne za juu ambazo zinatoa uwakilishi kwenye michuano ya kimataifa.

Ruvu Shooting yenye pointi 15 haipo katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi na inatakiwa ifanye kazi ya ziada kujinusuru.



Masau Bwire

## *Simba yawaandalia 'Suprise' Waarabu*

INATOKA UK 24

mazuri, tunajua mpira wa barani Afrika umebadilika, lakini timu za Afrika Kaskazini ambazo tunaziita za Kiarabu hadi leo bado hazijabadilisha mfumo wao wa uchezaji, bado kwa kiasi kikubwa sana wanategemea kushinda kwenye viwanja vyao vya nyumbani, Al Ahly, pamoja na ubora wake wote, huwezi kuona ubora wake wa asilimia 100 wakiwa viwanja vya ugenini, labda kama ametanguliwa kufungwa ndiyo unamwona anaanza kufurukuta na kututumka.

Akirudisha bao anarudi tena kwenye aina yake ya uchezaji wa taratibu na kupoteza muda, mechi yake anayotegemea ni ile ya nyumbani. Hivyo hivyo kwa Raja Casablanca, hatutegemei kama anaweza kuja hapa akacheza kwa kasi kubwa kama anavyocheza kwao, lakini vyovyote itakavyokuwa sisi Simba tumejidhatiti iwavyo ilivyo, tuhangaike naye kuanzia dakika ya kwanza hadi 90 kwa kasi ya hali ya juu, tumepelekee moto kweli kweli, mwisho wa siku tupate pointi tatu," alisema Ahmed.

Simba ambayo ipo katika Kundi C, inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza kwa bao 1-0 ugenini dhidi ya Horoya ya Guinea, wakati vinara wa kundi hilo wataingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kuitwanga Vipers SC ya Uganda mabao 5-0.

## Nabi: Yanga tuna njaa ya mafanikio

INATOKA UK 24

kwa dakika 20," alisema Nabi.

Aliongeza licha ya kupoteza mechi huko Tunisia, bado anawaamini mabeki wake waliopo ambao ni Yannick Bangala, Bakari Mwamnyeto na Dickson Job.

Wakati huo huo Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amesema suala la kiungo wao Feisal Salum 'Fei Toto' liko vizuri na keshokutwa atakuwa miongoni mwa wachezaji watakaokuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Fei Toto ni mchezaji halali wa Yanga, suala la yuko kambini au hayupo, Jumapili tutakapocheza dhidi ya TP Mazembe, atakuwa sehemu ya wachezaji wote uwanjani," alisema Kamwe na kuwataka mashabiki kujitokeza kwa wingi katika mechi hiyo.

Kauli hiyo ya Yanga imekuja baada ya gazeti hili kuandika sintofahamu iliyokuwapo kati ya klabu hiyo na Fei Toto imemalizika na Mzanzibari huyo amesaini mkataba mpya wa miaka miwili.

Inadaiwa Fei Toto amelipwa Sh. milioni 350 ili kusaini mkataba huo na sasa atapokea mshahara wa Sh. milioni 15 kwa mwezi.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/02/23 | 18:00 | Blackpool vs Stoke City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 02. 18/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Birmingham City | 2.65 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 18/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Leeds United | 2.36 | 3.30 | 2.95 |
| 04. 18/02/23 | 18:00 | Hull City vs Preston North End | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 05. 18/02/23 | 18:30 | Portimonense SC vs Maritimo Madeira | 2.29 | 3.15 | 3.15 |
| 06. 18/02/23 | 20:00 | FC Winterthur vs FC Sion | 2.45 | 3.10 | 2.44 |
| 07. 18/02/23 | 20:30 | CD Leganes vs UD Las Palmas | 2.70 | 2.90 | 2.80 |
| 08. 18/02/23 | 20:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.27 | 3.45 | 2.95 |
| 09. 18/02/23 | 20:30 | RCD Mallorca vs Villarreal CF | 3.15 | 2.95 | 2.42 |
| 10. 18/02/23 | 20:45 | FC Groningen vs FC Emmen | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 11. 19/02/23 | 14:15 | SC Cambuur vs SC Heerenveen | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 19/02/23 | 15:00 | Motherwell FC vs Heart of Midlothian FC | 2.80 | 3.25 | 2.47 |
| 13. 19/02/23 | 16:00 | SD Huesca vs Granada CF | 3.30 | 2.95 | 2.34 |
| 14. 19/02/23 | 16:00 | Elche CF vs Espanyol Barcelona | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 15. 19/02/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Montpellier HSC | 2.50 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 19/02/23 | 18:15 | Rayo Vallecano vs Sevilla FC | 2.43 | 3.00 | 3.05 |
| 17. 19/02/23 | 18:30 | Santa Clara Azores vs FC Famalicao | 2.80 | 3.15 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 17/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2570 | PSS Sleman vs Dewa United | 3.36 | 3.21 | 2.04 |
| 13:00 | 3967 | Kawasaki Frontale vs Yokohama F Marinos | 2.40 | 3.37 | 2.59 |
| 14:00 | 4756 | Tiddim Road Athlectic Club vs Aizawl FC | 2.09 | 3.21 | 3.21 |
| 16:00 | 1319 | Hawassa Kenema SC vs Bahir Dar Kenema FC | 3.52 | 2.85 | 2.15 |
| 16:00 | 3048 | Geita Gold FC vs Ruvu Shooting | 1.73 | 3.22 | 4.78 |
| 16:30 | 5629 | Ittihad Kalba vs Al Ain | 5.40 | 4.15 | 1.48 |
| 17:00 | 1244 | Northeast United FC vs Delhi Dynamos FC | 4.55 | 4.09 | 1.57 |
| 18:00 | 2064 | Chindia Targoviste vs Universitatea Cluj | 2.69 | 2.85 | 2.80 |
| 18:00 | 3668 | Al Nasr Riyadh vs Al Taawon | 1.56 | 3.94 | 5.76 |
| 19:00 | 3126 | Slaven Belupo vs HNK Sibenik | 2.04 | 3.11 | 3.47 |
| 19:00 | 4352 | Fasil Kenema vs Ethiopia Electricity | 2.14 | 2.90 | 3.47 |
| 19:15 | 2173 | Al Wasl Dubai vs Al Nasr Dubai | 2.13 | 3.36 | 3.00 |
| 19:30 | 5908 | Spartak Trnava vs Ruzomberok | 1.74 | 3.46 | 4.24 |
| 20:30 | 1017 | Eintracht Braunschweig vs Holstein Kiel | 2.82 | 3.46 | 2.29 |
| 20:30 | 1178 | Orlando Pirates vs Maritzburg Utd | 1.82 | 3.28 | 4.44 |
| 20:30 | 4906 | Paderborn vs Kaiserslautern | 1.84 | 3.67 | 3.77 |
| 21:00 | 3859 | FC Helsingor vs HB Koge | 2.12 | 3.32 | 3.06 |
| 21:00 | 4141 | CS Mioveni vs Rapid Bucuresti | 3.75 | 3.17 | 2.01 |
| 21:00 | 4778 | Wehen vs Erzgebirge Aue | 1.72 | 3.59 | 4.54 |
| 21:00 | 5480 | Aalborg vs Aarhus | 2.84 | 3.34 | 2.36 |
| 21:00 | 5796 | Tondela vs Viseu | 2.63 | 3.10 | 2.62 |
| 21:30 | 1002 | Yverdon-Sport FC vs FC Vaduz | 2.06 | 3.47 | 3.06 |
| 21:30 | 1123 | Bourg Peronnas vs Chateauroux | 2.62 | 3.10 | 2.63 |
| 21:30 | 1183 | FC Wil vs Neuchatel Xamax | 1.79 | 3.62 | 3.78 |
| 21:30 | 2559 | Le Mans vs Nancy | 2.09 | 3.14 | 3.46 |
| 21:30 | 4637 | FC Schaffhausen vs FC Aarau | 2.56 | 3.42 | 2.40 |
| 22:00 | 1186 | ADO Den Haag vs PEC Zwolle | 3.68 | 3.79 | 1.82 |
| 22:00 | 2060 | Dordrecht vs VVV Venlo | 2.89 | 3.37 | 2.26 |
| 22:00 | 2657 | Jong AZ Alkmaar vs Den Bosch | 2.05 | 3.45 | 3.25 |
| 22:00 | 4433 | Telstar vs Jong PSV | 2.00 | 3.41 | 3.41 |
| 22:00 | 4740 | FC Oss vs FC Eindhoven | 3.14 | 3.30 | 2.16 |
| 22:00 | 5503 | Waalwick vs Fortuna Sittard | 2.20 | 3.41 | 3.02 |
| 22:00 | 5836 | Almere City vs Helmond Sport | 1.57 | 3.93 | 5.14 |
| 22:15 | 2714 | FC Thun vs FC Stade LS Ouchy | 2.04 | 3.41 | 3.15 |
| 22:30 | 4295 | Augsburg vs Hoffenheim | 2.63 | 3.43 | 2.45 |
| 22:30 | 5565 | Pisa vs Venezia | 2.16 | 3.11 | 3.38 |
| 22:45 | 1577 | Ballymena Utd vs Glentoran Belfast | 5.40 | 4.00 | 1.50 |
| 22:45 | 1664 | Dundalk FC vs UCD Dublin | 1.31 | 4.78 | 7.89 |
| 22:45 | 3640 | Sassuolo vs Napoli | 5.18 | 4.18 | 1.54 |
| 22:45 | 3746 | Morton vs Dundee FC | 3.21 | 3.21 | 2.16 |
| 22:45 | 3896 | Mechelen vs Racing Genk | 4.19 | 3.79 | 1.75 |
| 22:45 | 4254 | Queens Park vs Raith Rovers | 1.92 | 3.47 | 3.62 |
| 22:45 | 4415 | Shelbourne vs Drogheda Utd | 1.56 | 3.73 | 5.18 |
| 22:45 | 4998 | Cork City vs Bohemians FC | 2.48 | 3.06 | 2.70 |
| 22:45 | 5788 | St Patricks vs Derry City | 2.55 | 3.11 | 2.59 |
| 23:00 | 1954 | Girona vs Almeria | 1.80 | 3.64 | 4.19 |
| 23:00 | 2115 | AJ Auxerre vs Lyon | 4.18 | 3.68 | 1.77 |
| 23:00 | 2948 | FC Cartagena vs Real Oviedo | 2.45 | 2.77 | 3.22 |
| 23:00 | 4099 | Cardiff vs Reading | 2.07 | 3.32 | 3.37 |
| 23:15 | 3396 | Gil Vicente vs FC Vizela | 2.41 | 3.39 | 2.74 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe

Ijumaa Februari 17, 2023




Arteta aeleza siri kuambulia kichapo

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto beki, Henock Inonga, Shomary Kapombe (katikati) na nahodha, John Bocco, wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba yawaandalia 'Suprise' Waarabu

## ●●● Robertinho afunguka kikosi chake kimejipanga kucheza kwa kasi ambayo...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Raja Casablanca kikitua mapema jana, Simba imesema maandalizi ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Waarabu hao kutoka Morocco yamekamilika na kilichobakia ni suala la muda.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, kikosi chake kitaingia kivingine kuwakaribisha wapinzani wao, Raja Casablanca kwa sababu wanahitaji ushindi na si matokeo mengine tofauti.

Robertinho alisema aina ya uchezaji ya ugenini na nyumbani huwa na tofauti kubwa, hivyo wamejiandaa kushambulia zaidi na amewaondoa hofu mashabiki wa timu hiyo.

Kocha huyo alisema anataka kuona vijana wake wakicheza kwa kasi kubwa dakika zote 90 ili kuhakikisha wanazibakisha pointi tatu nyumbani.

Alieleza walipocheza dhidi ya Horoya AC aliwataka wachezaji kujilinda na kushambulia kidogo na baada ya kufungwa bao pekee katika mchezo huo walifunguka kwa kuwashambulia wenyeji ili kusaka goli la kusawazisha.

"Nimepanga kuifanyia maboresho safu ya ushambuliaji inayoongozwa na Moses Phiri, John Bocco, Jean Baleke, Pape Sakho, Clatous Chama na Kibu Denis ili kuhakikisha wanapata ushindi wa mabao mengi nyumbani. Nataka kuona wachezaji wangu wakilishambulia goli la mpinzani wetu mara nyingi zaidi kwa maana ya kuanzia dakika ya kwanza hadi 90, kila mchezo wa nyumbani," alisema Robertinho.

Alisema hatua waliyofika katika mashindano hayo kila timu inatakiwa kupambana kupata ushindi nyumbani na kutafuta sare ugenini.

"Tunahitaji matokeo ya ushindi katika mchezo dhidi ya Raja Casablanca, kupata matokeo hayo tutalazimika kuingia na mbinu tofauti na tulivyoingia kwenye mechi iliyopita," Robertinho alisema.

Wakati huo huo, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema klabu yao jana iliwapokea maofisa kutoka CAF kwa ajili ya ukaguzi wa miundo mbinu kuelekea michuano ya Super League.

"Maofisa hao watakagua maeneo yote muhimu yanayohitajika kwa ajili ya michuano hiyo kama viwanja vya mazoezi, uwanja wa mchezo pamoja na hoteli. Uongozi wa klabu umewapa ushirikiano mkubwa ili kukamilisha kazi yao kwa haraka kwa muda unaotakiwa," aliongeza Ahmed.

Kuelekea mechi dhidi ya Raja Casablanca, Ahmed alisema wataingia kwa tahadhari katika mechi hiyo, ingawa haamini kama wapinzani wao watabadilisha mfumo ambao wamezoea kuucheza.

"Tahadhari ni muhimu, mchezo ni mgumu, ila sisi tunakwenda kutafuta matokeo

INAENDELEA UK 23

# Nabi: Yanga tuna njaa ya mafanikio

**Na Saada Akida**

AKILI na mawazo ya Yanga kuelekea mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ni kuhakikisha inapata ushindi wa aina yoyote na kufufua matumaini ya kusonga mbele kwenye mashindano hayo ya kimataifa.

Yanga inatarajia kuikaribisha TP Mazembe katika mechi ya Kundi D itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema timu yake itashuka dimbani kucheza mechi ya pili ya Kombe la Shirikisho Afrika ikiwa na njaa ya mafanikio.

Nabi alisema wamejiandaa kisaikolojia kuhakikisha wanapata matokeo chanya ili kufikia malengo ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kocha huyo alisema wanafahamu mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa pande zote mbili lakini wana matumaini watatumia vizuri uwanja wa nyumbani.

"Sioni kama tunastahili kufanya makosa kama yale tuliofanya Tunisia, tunajua mechi haitakuwa rahisi, tunakwenda kukutana na timu nyingine bora lakini tunapaswa kucheza kama Yanga yenye njaa ya mafanikio, wao wametoka kushinda mchezo wa kwanza, hivyo ari yao itakuwa juu," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza amewaangalia vizuri TP Mazembe katika mechi zake mbalimbali na kuona ubora pamoja na madhaifu yao, hivyo atahakikisha anafanyia kazi ili kufanikisha malengo ya timu yake.

Aliongeza hawatarajii kurudia makosa waliyofanya katika mchezo wa kwanza uliochezwa ugenini Tunis ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi mipira ya Set Pieces ambayo walifungwa na US Monastir.

Kuhusu beki wao mpya, Mamodou Doumbia, alisema sio kila mchezaji anayesajiliwa na timu hiyo ataingia katika kikosi moja kwa moja na badala yake anahitaji 'kumpika' taratibu mpaka atakapofahamu falsafa za timu hiyo.

"Huyu sio mshambuliaji ambaye anaweza kuja na kumpa nafasi haraka, nafasi ambazo mchezaji anaweza kuja na ukaona uwezekano wa kumpa nafasi ya kucheza hata kwa

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >